# *Ile Ishara*

Kusomwa kwa Neno. Kwa ajili ya ibada ya kumalizia, sababu yangu ya kuwaomba msimame. . .Wakati wanapoimba *Bendera Iliyopambwa Kwa Nyota*, mnasimama. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Naam."—Mh.] Basi kwa nini msisimame kwa ajili ya Neno la Mungu? Ni heshima. Sasa katika Kitabu cha Kutoka, mlango wa 12, kuanzia kwenye kifungu cha 12, ningependa kusoma sehemu ya Maandiko, kifungu cha 12 na 13.

> *Maana nitapita kati ya nchi ya Misri usiku huu, nami nitawapiga. . .wazaliwa wote wa kwanza katika nchi ya—ya Misri, wa mwanadamu na wa wanyama; nami. . .nitafanya hukumu; Mimi ndimi* BWANA.
>
> *Na ile damu itakuwa ishara* kwenu *katika zile* nyumba *mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, lisiwapate pigo lolote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri.*

2 Somo langu ni: *Ile Ishara*.

3 Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa. Na katika utulivu Wake wa wakati huu uliowekwa wakfu, kabla ya kumkaribia Yeye katika maombi, je! kuna haja ambayo ungependa Mungu ajibu alasiri ya leo? Inueni tu mikono yenu kama mnazo, na uwazie moyoni mwako kile unachotaka akufanyie. Popote kwenye jengo, wazia tu kile unachotaka akufanyie.

4 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe ni Mungu asiyebadilika, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utayajibu maombi yetu, alasiri ya leo, huku—huku tumeshikana mikono. Na Wewe unatambua kwamba mikono yangu imeinuliwa, pia. Na haja yangu, nitaifanya ijulikane wazi, Bwana, hiyo ni, kwamba utamponya kila mtu humu ndani leo hii, uokoe kila mmoja aliyepotea. Sasa, Wewe ulisema, "Mkimwomba Baba lolote, katika Jina Langu, nitalifanya." Sasa, Bwana, tusaidie pamoja kuamini kama kundi moja la watu, la watoto wanaoamini. Nena kupitia Neno Lako, Bwana. Neno Lako ni Kweli. Ibariki mioyo yetu.

5 Tunakushukuru kwa ajili ya mkutano huu. Tunakushukuru kwa ajili ya Ndugu Grant, na kwa ajili ya wafanyakazi wake wote, na makanisa yote na watu. Na kwa yote ambayo Wewe umetutendea, Bwana, tunakushukuru Wewe. Baba, huenda kuna wengi wetu hapa ambao hatutaonana mmoja na mwenzake tena sasa, mpaka tuweze kuonana upande ule mwingine. Huenda hii ikawa ndiyo ibada ya mwisho ambayo tutapata kukaa pamoja katika dunia hii. Jalia Roho mtakatifu aje na kutubariki pamoja, atupe haja zetu. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

Mwaweza kuketi.

6 Nina kijipande kidogo cha karatasi hapa, nimeandika baadhi ya Maandiko na mambo madogo. Ilikuwa kwamba ningeweza kukumbuka akilini mwangu, bali nimepita tu ishirini na mitano, mwajua, hiyo ni, mara ya pili. Na basi sikumbuki jinsi nilivyokuwa nikifanya, na mengi yamefungamana kwenye mikutano na kadhalika, na mengi sana ya kufanya.

7 Somo letu alasiri ya leo ni: *Ile Ishara*. Onyesho letu linafunguka huko Misri. Ni picha kuu hapa sasa, ninawatakeni nyote kuiona na mwe tu na kicho mwezavyo. Misri ndipo mahali pa tukio, na wakati wa tukio ni mwanzoni tu mwa kutoka.

8 Na, sasa, ni mfano wa leo hii, ulioonyeshwa, kama vile sisi pia tunakabili kutoka kwingine. Mungu akileta Israeli kutoka Misri, kuja kwenye nchi ya ahadi, kulikuwa ni mfano wa Kristo akimtoa Bibi-arusi kutoka kwenye kanisa, kuingia katika Nchi ya ahadi. Tuko kwenye kutoka kwingine. Sasa kama utachunguza Maandiko, tuna muda tu wa kugusia sehemu muhimu za hilo, hiyo ni kweli. Sisi ndio . . . Kama vile Mungu alivyolitoa taifa kutoka katika taifa, Mungu atamtoa Bibi-arusi kutoka kwa kanisa. Bibi-arusi ataitwa kutoka kwa makanisa yote. Atakuwa ni mteule wa Mungu, atakayetolewa. Nasi tuko kwenye ukingo wa kutoka huko sasa hivi, kwa kuwa tuna kila thibitisho la Kimaandiko kwamba tumesimama hapo. Sasa, ninajua hayo yamesemwa mara nyingi, bali, ewe rafiki yangu, siku moja litasemwa kwa mara ya mwisho. Wakati utatoweka kuingia katika Umilele wakati huo. Yeye anakuja kuchukua Bibi-arusi kutoka kwa kanisa.

9 Ishara ndiyo kitu kilicholeta tofauti kati ya Misri na Israeli, hayo mataifa mawili. Wote walikuwa ni wanadamu, lakini wote wameumbwa na Mungu, wote ni kazi ya mkono wa Mungu, ila, tofauti wakati adhabu ya kifo ilipopitishwa, tofauti kati ya uhai na mauti ilikuwa ni ile ishara.

10 Na ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Mungu, wakati atakapomtoa Bibi-arusi kutoka kwa kanisa, tofauti itakuwa ni ile Ishara. Sasa, nyinyi sikilizeni kwa makini alasiri ya leo, na mwone kama hiyo si kweli. Ishara itakuwa ndiyo tofauti. Hapana budi kuwepo na tofauti.

11 Mungu anaenda kuuhukumu ulimwengu, siku moja. Kama ningaliuliza watu Wakatoliki, ni kwa nani Yeye atauhukumu, ni kitu gani atakachouhukumu ulimwengu kwacho? Wangalisema, "kanisa." Kanisa gani? "Kanisa Katoliki." Kanisa Katoliki ipi, yapo kadha? Wamethodisti wangesema, "kwa la Methodisti," Wabaptisti wako nje basi. Basi, kama ukiuhukumu kwa kanisa la Kibaptisti, wengine wote wako nje. Wapentekoste wanasema, "kwa la Pentekoste," basi hayo mengine yako nje. Unaona, ingekuwa mchafuko, mchafuko mwingi sana, unaochanganyisha sana akili, kuwazia jambo kama hilo.

12 Bali Mungu alikuwa na njia hapa ambayo alisema alikuwa anaenda kutumia kuihukumu dunia, si kwa kanisa Katoliki, si kwa kanisa la kiprotestanti. Bali anaenda kuuhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo, naye Yesu ni Neno, kwa hiyo hapo inarudi kwenye Biblia tena. Mnaona? Atauhukumu ulimwengu kwa Biblia. Nayo Biblia ndiyo Kitabu cha Mungu cha Hukumu, ambacho ni ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo, ambacho hakuna kitu kingine kinachoweza kuongezwa wala kuondolewa Kwake; adhabu ya kufanya hivyo, ni jina lako kuondolewa kutoka kwenye Kitabu cha Uzima. Dumu tu moja kwa moja ndani ya Kitabu, na umwombe Mungu atufanye sehemu ya Hicho.

13 Sasa tunaona, ishara, ishara ni nini? Ishara ni ushahidi wa gharama iliyolipwa, ndiyo ishara. Kama tu vile usafiri wa garimoshi na mabasi, tunachukua fedha zetu na kwenda kwenye stesheni. Sasa, unaona, kampuni ya basi hairuhusiwi, katika sehemu ambazo ishara zinatumiwa, hawaruhusiwi kuchukua fedha. Hawawezi kuchukua fedha, inahitaji ishara; tuseme, ndege, na mengine. Unaenda mahali fulani, kaunta ya kununulia, na kununua, kutokana na pesa zako, ishara kadha, ishara hii fulani. Nayo ishara hii ni ushahidi kwamba nauli yako imelipwa. Una haki kuabiri meli hiyo, kuabiri ndege, kuabiri basi, au chochote kile, mradi tu unashikilia ishara hiyo kuonyesha kwamba ninii—kwamba safari yako imelipiwa. Sasa kumbukeni jambo hilo. Msilisahau.

14 Mwana-kondoo aliyechinjwa wa Israeli alikuwa ndiye. . . alikuwa ndiye matakwa ya Mungu. Yehova alihitaji mwana-kondoo aliyechinjwa, mbadala asiye na hatia. Kama ambavyo tumekuwa tukipitia katika juma ambalo limepita sasa, kwamba Mungu, anapofanya uamuzi, kamwe haubadilishi. Naye alifanya njia, kitu Chake cha kwanza alichofanya wakati mwanadamu alipokuwa ameanguka, ilimbidi Yeye kumtengenezea njia ya kurudi, kama kweli alitaka kumkomboa, ndipo Yeye akafanya uamuzi kwamba alimkomboa mwanadamu kwa Damu ya Yule asiye na hatia. Naye daima amefanya jambo lilo hilo. Hajalibadilisha kamwe. Hakuna mahali ambapo Mungu atawahi kukutana na mwabuduo, ila tu chini ya Damu. Hapo ndipo mahali Pake pa pekee.

15 Tunajaribu kumfanya akutane chini ya theolojia yetu, chini ya dhehebu letu, chini ya mifumo yetu ya elimu. Wengine wamejenga minara na wengine wakajenga miji, Babeli na—na mnara wa Babeli, na namna zote za vitu mbalimbali. Bali ingali inabaki, Mungu hukutana tu na mwabuduo wa kweli chini ya Damu. Kamwe habadilishi hiyo. Hatuwezi kuwa Methodisti sisi sote, hatuwezi kuwa sote Wapentekoste, hatuwezi sote kuwa *hiki*, *kile*, au *kinginecho*, hatutakubaliana. Lakini nikimjia mtu, acha awe ni kasisi wa Katoliki au chochote alicho, akiwa chini ya Damu hiyo sisi ni ndugu, sijali mahali alipo, mradi tu yuko chini ya hiyo Damu.

16 Sasa, mwana-kondoo aliyechinjwa wa Israeli alikuwa ndiye aliyehitajiwa na Yehova, nayo damu ilikuwa ndiyo ishara ya kwamba kazi ilikuwa imefanywa. Mungu alihitaji kwa ajili ya ukombozi, kutoka Misri, kwenda kwenye nchi ya ahadi, alihitaji mnyama aliyechinjwa. Naye mnyama huyo ni sharti awe na . . . Damu ya mnyama aliyekufa sharti iwekwe juu ya kizingiti na juu ya mlango, na hiyo ilisimama kwa ajili ya ishara ya kwamba kile ambacho Yehova alihitaji kilikuwa kimetimizwa. Mnaona? Sasa, mwana-kondoo siye aliyekuwa ishara, damu ilikuwa ndiyo ishara. Sasa, uhai ulikuwa umetoka ndani ya kafara hiyo, na sasa damu ilikuwa ndiyo ishara. Amri zake zilikuwa zimetekelezwa. Damu ilisimama kwa ajili ya ishara, ushahidi kwamba mwaminio huyu alikuwa ametenda hasa kile kilichohitajika. Hiyo ndiyo ilikuwa ishara. Vema, kumwona mwaminio huyo, akiabudu, basi alitambulishwa na kafara yake. Unaona?

17 Hii *hapa* nyumba, naye mwabuduo, ni kitu gani kilichohitajika? “Chinja mwana-kondoo. Kwenye siku ya kumi na nne baada ya kuwekwa, du—dume asiye na waa, Israeli yote itamchinja, na damu itatwaliwa na hisopo na kuwekwa kwenye kizingiti cha mlango.”

18 Pia, jambo jingine, hiyo hisopo ilikuwa tu ni mmea wa kawaida. *Hisopo* maana yake “imani yako.” Mtu fulani anajaribu kuwa na imani ya kimbinguni, hiyo ndiyo sababu unakosa uponyaji wako. Imani ni kitu cha kawaida tu. Unayo imani kuja kanisani. Unayo imani kutembea huko nje. Unayo imani kuwasha gari lako. Unayo imani kula chakula chako cha jioni. Hivyo ndivyo ilivyo, imani ya kawaida tu. Sasa kuweka damu, iliwekwa na hisopo, ambao ni mmea wa kawaida tu unaomea mahali popote Palestina, ukionyesha kwamba imani ambayo kwayo damu inafaa kuwekwa si kitu fulani cha juu ambacho inakubidi kuwa na kila namna ya digrii za udaktari kulifanya. Ni ya kawaida tu, imani ya kila siku, kumwamini Mungu. Unaona? “Iweke damu,” kwa imani, “na hisopo.”

19 Sasa, mwabuduo, basi, akionekana chini ya damu hii, ilionyesha kwamba alikuwa ametekeleza amri ya Yehova, naye alitambulishwa. Ishara ilionyesha alitambulishwa na mwana-kondoo aliyechinjwa ambaye Yehova alihitaji. Kazi ilikuwa imefanywa. Ni mfano mkamilifu jinsi gani leo hii, wa Kristo na mwaminio. Ishara ikionyeshwa kwa mwaminio, basi Hiyo inaonyesha kwamba imekubalika na kazi imefanywa.

20 Halafu, damu ilikuwa ni ishara ya utambulisho, damu yenyewe. Mnyama alitokwa damu, akafa, nayo damu yake ilikuwa ukutani. Sasa, uhai wa mnyama, uliokuwa ndani ya damu. Na uhai umo katika damu, tunajua hilo. Biblia ilisema hivyo, nayo sayansi inathibitisha hilo, uhai umo katika damu. Kwa hiyo basi wakati huyo mnyama alipouawa, nao uhai ukavunjwa kutoka kwa mnyama huyo, damu hiyo ilibidi iwe ni

kemia ya damu, kusimama kwa ajili ya ishara. Kwa sababu, uhai uliokuwa katika damu haungeweza kurudi juu ya mwaminio, kwa sababu ulikuwa ni uhai wa mnyama.

21 Basi uhai wa mnyama na uhai wa mwanadamu ni tofauti kabisa. Hakuna, hakuna chochote ndani yake hata kidogo. Ulichukua, chukua damu ya mnyama na kuweka ndani yako, utakufa. Kwa hiyo unaona, sisi, ni—ni uhai tofauti katika damu ya mnyama tofauti na ulio katika damu ya mwanadamu, kwa sababu mwanadamu anayo nafsi. Mnyama hana nafsi.

22 Ndipo sasa, basi, damu yenyewe, elewa sasa, kemia nyekundu, kemikali za damu, ilibidi zisimame juu ya mlango, kama ishara kwamba mwana-kondoo alikuwa amekufa, sasa, kwa sababu uhai wa mwana-kondoo usingeweza kurudi juu ya mwanadamu mwabuduo. Bali leo hii . . . Hiyo ilikuwa tu ni mfano.

23 Leo hii si kemikali ya Damu ya Bwana Yesu, Mwana-kondoo wetu, bali ni Uhai uliokuwa katika Damu, ambao ni Roho Mtakatifu. Unarudi na ndiyo ishara kwamba tumekubali na kufanya hasa kile Mungu alichotuambia kufanya. Halafu basi, kwa kuwa na Ishara, tunatambulishwa na Kafara yetu. Kikamilifu. Sioni jinsi ambavyo kitu chochote zaidi kingeweza kuwa wazi zaidi. Mnaona?

24 Njia ya pekee ambayo mtu yeyote angeweza kujua kwamba nyumba hiyo ilikuwa, pia, chini ya damu, kwa sababu kemia ya damu ilikuwa kwenye milango. Walipitia, Malaika wa mauti ilibidi aangalie na kuona damu. Sasa, tena, ilikuwa ni mfano wa Roho Mtakatifu.

25 Sasa, unaona, Damu halisi ya Yesu isingeweza kuja juu ya kila mmoja wetu, kwa sababu alikuwa tu na kiasi fulani cha Damu mwilini Mwake. Na ilidondoka, kutoka kwa mwili Wake, ikaanguka ardhini, miaka elfu mbili iliyopita; bali haikuwa iwe kwa ajili ya Ishara. Uhai, Uhai uliokuwa katika Damu, ulikuwa ndio Ishara sasa. Nitawathibitishieni, kwa dakika moja, kwa Biblia. Ndio Ishara ambayo inafaa kuja juu ya kila mmoja wetu, kuonyesha kwamba tumetambulishwa na Kafara yetu, na tumetekeleza amri ya Yehova.

26 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, wale wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita." Mnaona, sio tu kuwaonyesha wao. "Wote wale ambao Bwana atawaita."

27 Wapo wengi wanaodhani kuwa wameitwa. Lakini wote "Bwana" awaitao! "Wale aliotangulia kuwajua, aliwaita; wote aliowaita, aliwahesabia haki; wote aliowahesabia haki, amewatukuza," tayari jambo hilo limetimizwa.

28 Ndipo basi unapomchukua mtu ambaye haamini kwamba Roho Mtakatifu ni wa siku hizi, unaona kile wanachofanya? Wanaikana Ishara ambayo ndiyo alama hasa ya wewe kuunganishwa na Kafara yako. Mnaona ninachomaanisha? Ni rahisi sana kama ukiiangalia tu katika—katika njia ambayo Mungu ameiandika sasa. Damu ilitubeba na sisi tulikuwa . . . inaonyesha m—mfano wa Roho Mtakatifu, ambao ni Uhai.

29 Sasa, uhai wa mnyama usingeweza kurudi ndani ya mwanadamu, kwa kuwa hazingepatana, uhai wa mnyama hauna nafsi ndani yake. Uhai wa mwanadamu una nafsi. Mnyama hajui kuwa yuko uchi. Hajui tofauti kati ya mema na mabaya. Yeye, yeye ananinii tu . . . Anayo ro—roho, bali si nafsi. Sasa kumbukeni, sasa, nafsi ni asili ya roho, bila shaka.

30 Sasa angalia, lakini basi wakati Uhai wa Kafara yetu, Yesu Kristo, wakati Damu Yake ilipomwagwa. Alikuwa ni Mungu, aliyefichwa ndani ya Mtu mmoja. Sasa, alishuka chini kutoka kuwa Yehova, ili kujitambulisha Mwenyewe kama mwanadamu, kujitwalia Mwenyewe umbo la mwanadamu, ili kututambulisha na Yeye. Yeye alikuwa ndiye Mwana-kondoo wa Mungu. Na ndani Yake, ambapo Damu . . .

31 Sasa ninajua mtu fulani anasema, "Yeye alikuwa ni damu ya Kiyahudi." Unawasikia Wayahudi wakisema hivyo. Hakuwa ni damu ya Kiyahudi, na wala hakuwa damu ya Mataifa. Yeye alikuwa ni Damu ya Mungu. Hakuwa na ya Kiyahudi wala . . . Hakuwa Myahudi wala Mataifa. Alikuwa ni Mungu. "Bi—bi—bikira atachukua mimba."

32 Sasa, ninajua wengi wenu enyi watu na Waprotestanti wanafikiri ya kwamba yai lilikuwa la Mariamu. Nayo hi—himoglobini ambayo hutoka, uhai hutoka kwenye seli ya damu. Kwa sababu, kuku anaweza kutaga yai, bila ya kuwa na ndege wa kiume, halitaanguliwa, kwa maana halijarutubishwa. Uhai hutoka kwa damu, ambayo hutoka kwa jinsia ya kiume. Lakini katika kisa hiki hakukuwa na jinsia ya kiume, kwa hiyo, "uhai katika damu," ilibidi itoke kwa Mungu pekee, na Yeye aliumba seli ya Damu katika tumbo la uzazi la Mariamu. Mungu Mwenyewe, Muumba Mwenyewe, aliumba seli ya Damu. Sasa angalia. Wanasema, "Vema, ulikuwa ni mwili. Mariamu alikuwa na yai." La, bwana. Hakuwa; hakuna yai. Kama lilikuwa ni yai, huwezi kupata mbegu ya kiume bila ya msisimko. Na kama Yeye, mwanamke alikuwa na msisimko, unamfanya Mungu kufanya nini?

33 Yeye aliumba yai na Damu pia. Hivyo ndivyo alivyokuwa hasa. "Tulimgusa Mungu," Biblia ilisema. Timotheo wa kwanza 3:16, "Bila shaka siri ya utauwa ni kuu: Mungu alidhihirishwa katika mwili. Tulimgusa kwa mikono yetu." Huo mwili ulikuwa Mungu. Hakika, ulikuwa. Alikuwa ni Mungu kote, katika umbo la mwanadamu.

34 Sasa tunaona katika hili, kwamba seli hiyo ya damu ikivunjwa, hiyo ilimwachilia Mungu. “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Ambapo, hakuna mwingine angaliweza kufanya hilo, hakuna kitu kingine kingaliweza kufanywa; ilihitaji hiyo Damu takatifu, Mwenyewe. Ilibidi Mungu ashuke na kufanyika mwanadamu, apate kuwajibishwa na sheria Yake Mwenyewe. Kama Yesu alikuwa tu ni nabii, mtu aliyetengwa na Mungu, basi Mungu si mwenye haki.

35 Kama ningaliweza kusema, “Acha Ndugu Grant afe kwa ajili ya dhambi fulani ambayo Billy anapaswa kufa kwa ajili yake, au kitu kingine, adhabu fulani,” hiyo isingalikuwa ya haki. Kama ningalimfanya mvulana wangu kufa kwa ajili ya adhabu ambayo mimi mwenyewe nilitangaza, bado si haki. Lipo jambo moja tu la haki ambalo ninaweza kufanya, hilo ni kuchukua mahali pake, ikiwa ninataka kumwokoa.

36 Naye Mungu ilibidi afanyike mwili, ili kwamba aweze kuchukua mahali pa mwenye dhambi; Mungu akidhihirishwa katika mwili, si kitu chochote pungufu ya Mungu Mwenyewe. Sasa, Huyu hapa alikuwa, akidhihirishwa katika mwili, kuondoa dhambi za ulimwengu. Naye alijitambulisha Mwenyewe ndani yetu, ili sisi tuweze kutambulishwa ndani Yake. Unaona kusudi lake?

37 Sasa tunaona utambulisho wetu na Kafara yetu, Uhai wa Kafara ndani yetu, ambao ni Roho Mtakatifu. Wakati seli hiyo ilipovunjwa, ilimwachilia Mungu, ilimwachilia Mungu, kwamba Yeye alikuwa amewatakasa watu kwa Damu Yake Mwenyewe na kumweka Mungu ndani ya mwanadamu tena. Mungu ndani yako, Uzima wa Milele!

38 Na msomi yeyote wa Kiyunani anajua kwamba neno hilo, Uzima wa Milele, linatokana na neno Z-o-e, *Zoe*, ambalo linamaanisha “Uhai wa Mungu Mwenyewe.” Hiyo ni kweli. Njia ya pekee ya kuweza kuwa na Uzima, kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo ni Uhai wa Mungu Mwenyewe ndani yako. Unaona? Ndipo una Uzima wa Milele, kwa sababu Yeye ndiye wa Milele wa pekee aliyepo. Nasi ni sifa za mawazo Yake, kabla ya kuwepo hata na msingi wa ulimwengu au chochote. Haya yote ni mawazo Yake tu, nasi ndio dhihirisho la mawazo Yake ya kile kilichokuwa.

39 Basi ilimbidi kushuka chini ili kuondoa dhambi. Hakuna mwingine angaliweza kufanya hilo. Hakuna aliyestahili kufanya hilo. Hakuna aliyeweza kulifanya isipokuwa Yeye, na Yeye alifanya hivyo. Ndipo basi wakati Uhai huo ulipoachiliwa kutoka kwa mwili huo, Mtu, ambaye alikuwa ni Mwana wa Mungu; nguvu Zake za uumbaji zilimjengea jengo, kama vile kontrakta yeyote, alijenga jengo ambalo alihamia, Mwenyewe. Mungu alifanya hilo.

40 Halafu basi wakati uhai huo ulipochukuliwa, ile Damu, kemia Yake, ikamwagwa juu ya nchi, kama tu vile ya Habili mwenye haki ilivyomwagwa juu ya nchi. Bali kutokana na hiyo Damu akaja Roho Mtakatifu wa Mungu, na huyo alitumwa kwa mwanadamu kwenye Siku ya Pentekoste, kutambulishwa na Kafara iliyokufa kwa ajili yao. Hakuna njia yoyote nyingine ulimwenguni tuwezayo kumpata. Ishara halisi!

41 Angalia, kama ulikuwa na hatia ya kufa, nawe ulijua ulikuwa unaenda katika kiti cha umeme. Pia kumbuka, kukataa . . .

42 Dallas, sikilizeni! Kuikataa Damu ya Yesu Kristo, Ishara ya Damu Yake, kama ukiiona na kuikataa, utakabili Hukumu na Damu Yake mkononi mwako. Mwenye dhambi, mshiriki wa kanisa, kumbuka hilo.

43 Vipi kama Lee Oswald angekuwa anaweza, siku hizo chache, na huko kutokwa jasho mbele ya Mahakama Kuu iliyompasa kuikabili; na alijua, kutokana na kumwua Rais, hakungekuwapo na hata chembe moja ya huruma, jinsi ambavyo hapana shaka mtu huyo alihisi! Hapana budi lilikuwa ni jambo la kutisha. Hakuwahi kulikabili, kwa sababu jamaa yule mwingine alimpiga risasi. Lakini hebu wazia juu ya kukaa pale mbele ya Mahakama Kuu yenye hasira, huku damu ya mwanadamu mwenzako iko mkononi mwako, Rais wa Marekani! Hilo litakuwa ni jambo dogo, kwenu enyi watu mnaoipita Damu ya Yesu Kristo, mtakaposimama mbele ya mahakama za Mungu. Toa jasho wakati unajua. Oswald asingalifanya zaidi ya kuondoka katika maisha haya kwake, lakini Mungu anakuondoa Milele kutoka Uweponi Mwake. Litakuwa ni jambo la kutisha. Angalia.

44 Kama ilikubidi kuja mahakamani, kwa kuwa na hatia, ungemtafuta wakili aliye bora kuliko wote uliyeweza kumpata. Mtu yeyote angefanya hivyo.

45 Na kila mtu aliyezaliwa ulimwenguni, sijali anatoka katika boma zuri namna gani, ana hatia ya Damu ya Yesu Kristo mpaka awe amekubali msamaha wake. Nayo njia ya pekee ya kujua kwamba msamaha ni sahihi, ni wakati Ishara inapojiweka Mwenyewe juu yako, nawe una Ishara.

46 Angalia, una hatia, na ungemtafuta wakili aliye hodari kuliko wote uliyeweza kumpata kuitetea kesi yako. Na kama nilikuwa ninaelekea kwenye Hukumu ya Mungu, sitaki kasisi yeyote, sitaki mwanadamu yeyote; ninataka wakili bora zaidi niwezaye kumpata kuitetea kesi yangu.

47 Hebu niseme kwa hili, kwako, ewe rafiki yangu Mkristo. Wakili wetu ndiye hakimu wetu pia, na hakimu we—wetu alifanyika wakili wetu. Kesi imeisha tukipokea msamaha Wake. Hakimu Mwenyewe alishuka chini akafanyika wakili, basi wakili na hakimu ni Mtu yule yule. Mungu alifanyika

mwanadamu, ili aweze kumhesabia haki mwanadamu kwa mauti Yake Mwenyewe aliyoweka juu yake. Haleluya! Hiyo inamaanisha, asifiwe Mungu wetu! Yeye anastahili sifa zote. Hakimu wetu na wakili wetu ni Mtu yule yule.

48 Roho Mtakatifu ndiye Ishara kwamba tumesamehewa. Kesi imefungwa. Kwa kila mwanamume na mwanamke ambaye kwa kweli amepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, amejaribiwa, ametambulishwa na wakili wake, na hakimu wake, na kafara yake, na Ishara aliyo nayo katika umiliki wake inaonyesha ya kwamba safari yake imelipiwa kwenda Utukufuni. Amina. Imekwisha. Anashikilia Ishara hiyo. Ni yake, ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambaye ndiye shahidi wa kufufuka kwa Yesu. Amina. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Huo ndio utambulisho wako, unashikilia Ishara.

49 Sasa ikiwa hujapata hiyo Ishara, hutaingia. Huna budi kuwa na Ishara. Hiyo ndiyo gharama inayohitajika, "Nionapo damu, damu ndiyo ishara. Nionapo damu, nitapita juu yako." Sharti uwe na Ishara. Kama huna, mbona, hutaenda. Huna budi kuwa na Ishara.

50 Iwapo ishara haikuonyeshwa, ishara haikuonyeshwa huko chini, hata agano halikufanya kazi. Unasema, "Vema, sasa, Ndugu Branham, sasa ngoja kidogo tu." Hiyo ni kweli kabisa.

51 Ishara ilikuwa juu ya agano. Kwa kuwa Israeli ilikuwa na agano kutahiriwa, na Myahudi yeyote angeweza kutoka na kuonyesha mtu yeyote, "Ninaweza kukuthibitishia nimetahiriwa, mimi ni Myahudi, nimetahiriwa kulingana na amri ya Yehova," lakini hata hivyo hiyo haikumweka huru kama ishara haikuwa pale pia. Hana budi kuonyesha ishara. Je! mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye... Ishara haina budi kuwepo, kwa vyovyote vile. Na iwapo uko kwenye agano...Kama Myahudi yeyote angesema, "Siweki damu yoyote mlangoni pangu, ninaweza kuthibitisha kwamba mimi ni Myahudi wa agano," Malaika wa mauti alimpata. Haidhuru jinsi alivyokuwa ni mwaminifu, jinsi alivyokuwa ni mfuasi wa kanisa, kiasi cha zaka alizotoa, jinsi alivyosema kwamba alimwamini Yehova; Yehova alihitaji hiyo ishara.

52 Naye anaihitaji leo hii, pia. Haina budi kuwa hivyo. Lazima iwe, "Kwa kuwa hakuna njia nyingine chini ya Mbingu, hakuna jina jingine lililotolewa kwa vyovyote," haijalishi jinsi ulivyo mwema, jinsi ulivyo mwaminifu. Ishara hiyo haina budi kuwepo, na kuonyeshwa.

53 "Damu," unasema, "vema, nilimwua mwana-kondoo na kuiweka katika jagi. Nimeiweka pale nyuma." Hilo silo alilosema. Sharti iwe juu ya kizingiti na mahali pa mlango. Haina budi kuwekwa hadharani.

54 Na maisha yako lazima yaonyeshe Ishara iko ndani yako. Loo, enyi Wapentekoste, mna shida gani? Nywele zilizokatwa,

nyuso zilizopakwa rangi, wanaume, mizaha michafu na kadhalika, kuko wapi kule kuonyeshwa kwa Damu ya Bwana wangu Yesu Kristo ndiyo Ishara ya Roho Mtakatifu? Ninyi, mkiwa na mfano wa utauwa, na kuita "uchawi" na kila kitu kingine, kazi za Mungu, "uchawi." Mnaonyeshaje ishara?

55 Wanasema, "Mimi ni Mpente-. . . " Sijali kile ulicho. "Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Pres-. . . " Sijali kile ulicho. Ishara hiyo sharti iwepo. Mungu anahitaji Hiyo, na si kitu kingine chochote ila hiyo.

56 Unasema, "Vema, ninayo ya udaktari." Sijali ni digrii ngapi ulizo nazo. Mungu anahitaji hiyo Ishara, na Hiyo pekee. Ni ushahidi ya kwamba safari yako imelipiwa. Hatachukua stakabadhi zako wala chochote kingine. Yeye hana budi kuipata hiyo Ishara.

57 Dereva wa basi anasema, "Hapa, ngoja kidogo, hiyo siyo ishara yangu."

58 Mtu wa ndege anasema, "Vema, wewe nenda huko nje sasa." Tikiti ni ishara. Wewe nenda huko nje ukamwambie rubani, "Hapa, nataka kuiabiri ndege yako. Ni pesa ngapi?"

"Ingia ndani ukanunue ishara yako."

"Loo, nitakulipa."

59 "Siwezi kuichukua. Hutaingia kwenye ndege yangu mpaka uende ulipe gharama na upate ishara. Mimi ninaangalia ishara."

Unasema, "Vema, nilienda shule. Nilifanya *hili*. Mimi . . . "

60 Sijali ulichofanya, sharti uwe na Ishara la sivyo huingii. Amina na amina. Hivi hamwezi kuona? Mungu anahitaji hiyo Ishara. "Nionapo damu, ndipo tu nitakapopita juu yako nionapo ishara."

61 Haikuwekwa hadharani, agano halikufanya kazi. Myahudi angeweza kusema hakika na kujithibitisha mwenyewe kuwa—kuwa ni Myahudi aliyetahiriwa, angeweza kuwapeleka kina ndugu nje na kusema, "Angalia hapa, nimetahiriwa." Hiyo haikumaanisha chochote.

62 Unasema, "Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni *hiki*. Mimi ni *kile*." Hiyo haimanishi chochote.

63 Huna budi kuwa na Ishara. Nayo Ishara ijapo, humshuhudia Kristo. Yeye alisema ingefanya hivyo. Naye Kristo ni Neno. Basi unawezaje kukataa kwamba Biblia ni sahihi, sehemu Yake, na bado useme una Ishara, huku Ishara ndiyo shahidi wa Yesu Kristo? Mnaona, hilo ndilo linalonishangaza.

64 "Loo," unasema, "Siamini, ninaamini siku za miujiza . . . " Loo, angalia, hakuna Ishara hapo. Ishara huitikia kila Neno kwa "amina," kila kitu, maana Yenyewe ni Mungu. Mnaona? Vema.

65 Lakini kama ishara haikuwepo, agano halikuwa na nguvu. Lilibatilishwa. Vivyo hivyo sasa! Haijalishi ni kiasi—ni kiasi gani unasema, ni kiasi gani ungesema, "Ninaamini kila Neno katika Biblia," useme, "Ndugu Branham, ni—ninaweza kunukuu nusu ya Biblia, Biblia nzima, kwa akili. Ninaamini kila sehemu yake." Hilo ni jema. Shetani anaamini, pia. A-ha. Inahiaji Ishara!

66 "Vema, Ndugu Branham, ukuta wangu umejaa digrii. Nina Digrii ya kwanza ya Sanaa, pia nina digrii ya udaktari, na LLD. ya Kilatini. Tena, loo, nimeandika vitabu. Nimefanya hili. Nimefanya kila kitu. Nime—nimefanya mambo haya yote." Sijali. Hayo yote ni sawa, lakini hata hivyo inakubidi uwe na Ishara. Ishara, Ishara bado inahitajika!

67 Unasema, "Mimi ni mwanafunzi wa Biblia. Mimi ni—mimi ni mtu mzuri. Mimi ni *hili*, *lile*." Hilo huenda likawa sawa, hayo yote ni mema, bali hata hivyo lazima iwe na Ishara!

68 Sasa, mauti yalikuwa tayari kuipiga Misri wakati wowote, na ndivyo mauti yalivyo tayari kulipiga taifa hili wakati wowote.

69 Anna Jeanne, ninahisi kitu kama baba yako, alivyotoa tamshi wakati mmoja. Daima nimelipenda hilo. Alisema, "Unajua, taifa hili, likiwa na dhambi zile zile, ikiwa Mungu ataiacha Marekani kuepuka pamoja na yale inayofanya, Yeye atawajibika kiadilifu kufufua Sodoma na Gomora na kuwaomba msamaha, kwa kuiteketeza." Na hiyo ni kweli.

70 Kumbukeni, Israeli ililipia kila dhambi iliyofanya, na vivyo hivyo nasi tutalipia. Tunakuwa walegevu jinsi gani? Fungeni silaha! Rudini kwa Mungu, enyi kanisa! Sisemi mambo haya ili kuwa tofauti. Ninawaambieni kama onyo. Nyinyi aminini!

71 Mauti yalikuwa tayari kupiga. Mungu alikuwa amewaonyesha neema Yake na rehema Yake, kupitia nguvu na ishara na maajabu (vivyo hivyo amefanya leo kabla ya kuliondoa Kanisa), wangali hawakutaka kutubu na kuamini ujumbe.

72 Mnaona, kulikuwako na ujumbe kabla tu ya kuondolewa kwa kanisa. Hauna budi kuwepo daima. Vivyo hivyo sasa. Kila tukio la kiroho ni ishara kutoka kwa Mungu. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kama vile ujumbe, kuna ishara halafu Ujumbe unafuata ishara. Mungu alimwambia Musa, kasema, "Ikiwa hawataamini sauti ya ishara ya kwanza, labda wataamini sauti ya ishara ya pili."

73 Sasa, mkiona ishara zikiendelea, na hakuna ujumbe nyuma yake, ni mwelekeo ule ule wa kale wa theolojia na kuendelea, hizo hazikutoka kwa Mungu. Lakini mahali palipo na ishara ikionyeshwa, Ujumbe unaifuata. Sasa angalia. Yesu alikuja jukwaani . . .

74 Je! ninawaziba masikio? Ama yeyote yule aliye kwenye maikrofoni hii hapa, inasikika kana kwamba inarudisha

mwangwi. Labda kidogo ina sauti kubwa kupita kiasi. Ninataka mlipate.

75 Wakati Yesu alipokuja jukwaani, Yeye hakusema mengi sana kwa watu, kila mtu alimtaka kanisani mwake. "Loo, Nabii huyu kijana, tuna furaha sana kuwa na Yeye." Alikuwa anawaponya wagonjwa. "Loo, utukufu kwa Mungu. Mungu amemwinua Mtu mashuhuri miongoni mwetu." Hilo lilikuwa jema. Basi siku moja ikafikia mahali ambapo . . . Hiyo ilikuwa ishara Yake.

76 Isaya 35 ilisema ingekuwa ni ishara. "Mtu aliye kilema atarukaruka kama kulungu," na kadhalika, "kipofu ataona." Ilikuwa ni ishara.

77 Alionyesha ishara Yake kama Masihi, na kadhalika. Na wao, wengi wao, walisema, "Naam, ninaweza kuendea hiyo." Vema, sasa, kama hiyo ilikuwa ni ishara, hapana budi pawepo na sauti ya ishara hiyo. Sauti nyuma yake ilikuwa ni nini? Wakati alipoanza kufundisha fundisho Lake na kuwaita kundi la nyoka katika nyasi. Hakuwa maarufu kuanzia hapo na kuendelea, unaona, wakati sauti ilipokuja na ishara. Ishara ilitangulia.

78 Musa aliienda huko chini Misri akiwa na ishara. Ndipo akatupa chini fimbo yake, ikageuka kuwa nyoka. Hiyo ilikuwa ni ishara. Lakini baada ya kitambo kidogo, sauti ikaja pamoja na ishara. Basi ikawa tofauti. Mnaona, hawataki hiyo. Sa— sauti, lazima iwe, ifuate ishara. Na hakuna wakati wowote ingaliweza kuja ila wakati huo, kwa sababu ulikuwa ni wakati wa Maandiko kutimia. Angalia kile alichomwambia, katika kichaka kilichowaka moto, "Nimeona kuugua na kusikia huko kwa watu Wangu, na kuona mateso yao kwa sababu ya wasimamizi wa Misri, Nami nimeikumbuka ahadi Yangu niliyomfanyia Ibrahimu." Miaka mia nne ilikuwa imekwisha, na Yeye alimwambia Ibrahimu wangekuwa huko chini. Mnaona, hakuna wakati wowote mwingine hilo lingekuwa. Ilibidi Musa aje tu kwenye wakati huo.

79 Saa kubwa ya Mungu huhesabu kikamilifu. Haitapitisha dakika moja wala kuwa dakika moja nyuma. Itakuwa tu kwa wakati kikamilifu. Vema, kwa hiyo, mnaona, kila kitu kilikuwa kinaenda tu sawasawa, asingeweza kuja kwenye nyakati zingine.

80 Wala mambo haya yasingeweza kuja nyakati zingine. Hili lisingeweza kuja katika siku za Luther. Lisingeweza kuja katika siku za Wesley. Siku za Baptisti ama Methodisti, katika siku zao, lisingeweza kuja. Halina budi kuja sasa. Israeli sharti liwe taifa. Makanisa ni sharti yawe jinsi yalivyo sasa. Ilibidi kuwe na ujumbe wa tatu, wakati wa tatu wa kanisa. Ilibidi kuwe na Laodikia. Haingeweza kuumbika mpaka Pentekoste iweze kuja na kufikia mwisho wao, na kwenda na kuunda dhehebu, na kufanya yale waliyofanya. Basi haina budi kuja, ndipo Bwana anakuja, wakati wamemweka nje ya kanisa. Yeye ni Neno.

81 Wanaogopa kukabiliana na Neno hilo mahali popote. Wananyamaza kimya kabisa kuhusu Hilo, lakini hata hivyo wanazozana kulihusu.

82 Chicago, hapa si muda mrefu uliopita, wakati Bwana aliponipa ono. Nilikuwa na wahudumu mia tatu huko chini. Nikasema, “Sasa ninajua kile nyinyi . . . Kuhusu uzao wa nyoka, na kadhalika,” nikasema, “mmoja wenu chukua Biblia yako na uje usimame karibu na mimi na ulikanushe.” Kundi nyamavu kuliko yote uliyowahi kusikia. Nikasema, “Basi niacheni.” Mnaona, ni kutokana na mafundisho yao.

83 Hata hivyo, wanasema, “Ndugu Branham ni nabii wakati akitiwa upako, lakini upako ukimwondokea, loo, sijui.” Ni ninii . . . Kama hiyo si alama ya mwa—mwa—mwa—mwanatheolojia aliyechanganyikiwa! Ninii hasa . . .

84 Neno *nabii* linamaanisha “mfunuaji wa Kiungu wa Neno.” Neno la Bwana liliwajia manabii. Hivyo ndivyo Yesu alivyotambulishwa. Na wao walisema baada ya ufufuo, walisema, “Sisi tunajua Yeye alikuwa ni nabii wa Mungu, mnaona, hakuna mtu angaliweza kutenda mambo haya, isipokuwa Mungu awe pamoja naye,” basi wasingalikubali ujumbe Wake. Wasingalimkubali Yohana, na yeye alikuwa ni nabii. Wasingalimpokea Eliya, si hata mmoja wa hao wengine, nao walikuwa na ufunuo wa Kiungu.

85 Neno, neno la Kiingereza, *nabii*, maneno ya Kiingereza yanaweza kumaanisha chochote, linamaanisha “mhubiri.” Lakini unaposema *nabii*, wa Biblia ya kale, lilimaanisha “mwonaji.” Na vitambulishi vyake vilikuwa, kile, yale aliyosema yakitimia, na hiyo ilikuwa ni ishara kwamba alikuwa ni nabii; yeye pia hiyo ilikuwa ni ishara ya kwamba alikuwa na ufunuo wa Kiungu wa Neno lililoandikwa. Halafu basi Mungu akilithibitisha, nyuma yake, lililihakikisha.

86 Vipi? Vema, inabidi tu iwe hivi, hivyo tu. Hamna njia ya kuihepa. Mungu alisema itakuwa hivyo, na haya basi. Bali hiyo hapo leo hii, unaona, hiyo Ishara haina budi kuwepo, inayolitambulisha Neno hilo na kulifanya kweli kabisa. Halafu jinsi Yeye alivyoliahidi, jinsi Yeye alivyowaandaa watu Wake wote wa nchi ya ahadi, sasa, wakati alipokuwa anaenda kuwa na huku kutoka, ambako kulikuwa ni mfano.

87 Sasa nitajaribu kuondoka kwa yapata dakika zingine kumi na tano, ishirini, pamoja na Ujumbe. Angalieni kwa makini sasa, ninawatakeni mpate hili, maana huenda nisiwaone tena, mnaona.

Angalieni, sasa angalieni jinsi Yeye alivyowaandaa watu Wake.

88 Ni wangapi wanajua kwamba Yeye kamwe habadilishi njia Zake? Kamwe habadilishi. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—

Mh.] Yeye ni . . . sasa angalia kupitia Biblia na uone kama aliwahi kuibadilisha. La, bwana.

89 Aliwaandaje watu? Kwanza, alimtuma nabii akiwa na ishara, ambaye alikuwa ni Musa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nayo ishara ilikuwa na ujumbe, ujumbe wa "iweni tayari," walikuwa wanatoka kwenda kwenye nchi iliyoahidiwa. Hapo Yeye alikuwa na utambulisho, wa nabii huyu, kwamba Nuru ilikuwa juu yake. Nguzo ya Moto ilimfuata nabii huyu, tunajua hiyo, ilipitia jangwani pamoja na Musa. Tunatambua hilo. Ndipo basi akawapa ishara kwa ajili ya hakikisho kwamba haikuwapasa kuogopa, kufadhaika na kuwa na wasiwasi; ambapo Yeye alisema, "Nionapo hiyo Ishara, nitapita juu yako."

90 Angalia jinsi alivyofanya sasa. Alitayarisha kwanza ishara, mjumbe, ujumbe uliotambulishwa, utambulisho wa mjumbe, na ishara kwa ajili ya hakikisho ya kwamba safari ilikuwa imelipiwa. Wanaelekea kwenye nchi ya ahadi.

91 Jambo lile lile amelitenda leo hii! Yeye alifanya nini? Alitutumia Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ndiye Mjumbe, na thibitisho la Kimaandiko la Yeye Mwenyewe akijitambulisha miongoni mwetu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Nayo ishara ndiyo hakikisho. Tunatishwa na nini? Nauli yetu ishalipwa tayari nasi tumetambulishwa na Kafara yetu. Hawezi kukukana. Aliahidi hilo. Tumetambulishwa.

92 Israeli wakitoka Misri, kama nilivyosema, ni kama Bi—Bibi-arusi akitoka kwa kanisa. Musa alipoanza huduma yake, Israeli wote walikusanyika Gosheni, kwa ajili ya maombi na ibada, hasa, walitoka sehemu zote za Misri. Hivyo ndivyo Bibi-arusi atakavyofanya, atatoka kwa wote wa Umoja, Uwili, Utatu, na aina zingine zote. Atatoka. Hana budi kutoka. Sasa tunasoma hapa katika Waebrania ninii . . . Sisi sasa, kitu cha kwanza kitupasacho kuwazia, kutoka sehemu zote, "Ondokeni miongoni mwa kutokuamini." Sasa Roho Mtakatifu aliahidi kumwita huyo katika siku za mwisho, "Tokeni miongoni mwa wasioamini." Angalia.

93 Tunaona katika Waebrania 10:26, nimeiandika hapa chini, inasema hivi, "Kama tukitenda dhambi makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, hakuna dhabihu tena kwa ajili ya dhambi," mnaona, ukikosa kuamini makusudi.

94 Sasa kama utaangalia, kile niwezacho kusema hapa, kama mtaniruhusu muda mfupi mpaka nitoe maelezo hayo. Ningeweza kuhisi katika roho, halikuingia vizuri. Mnaona? Angalieni.

95 Hawa hapa Wayahudi, wako njiani mwao wakitoka. Mungu aliwachagua watu kumi na wawili, ama Musa alichagua, kwa mkono wa Mungu, kuvuka na kwenda kupeleleza nchi; kisha warudi, walete ishara ya nchi hiyo. Basi walipofika huko, kumi kati yao waliogopa sana. "Mbona," walisema, "hao Waamaleki

huko juu, tunaonekana kama panzi kwao." Yoshua na Kalebu wakarudi, wakileta thibitisho, "Tunaweza!"

96 Mnaona, hao ni waaminio wakwamia mpakani. Wanapitia mambo haya mbalimbali, na kupitia kanisa, na kujiunga na kanisa, na mabatizo na desturi. Bali inapofikia moja kwa moja kwenye kuvuka ili kuipata ile Ishara, thibitisho kwamba Nchi ipo, kwamba Uhai . . . Yesu Kristo hajafa. Ni kiwango kingine. Yeye huishi kwa hicho. Yupo pamoja nasi, Yeye yumo ndani yetu sasa. Inapofikia hilo, "ah," wasingeliamini hilo. Hilo lilikiuka mpaka, unaona. Nao wakarudi, na wao, kila mmoja, alikufa nyikani, hakuna hata mmoja wao aliyevuka. Basi, unaona, tukikosa kuamini, sisi Wamethodisti, Baptisti, Presbiteri!

97 Natumaini mwalimu wangu wa kale ameketi hapa leo. Daktari Roy E. Davis, wengi wenu mnamjua, papa hapa Fort Worth, labda ameketi humu ndani. Nakumbuka tulijadili mambo haya, miaka mingi, mingi sana iliyopita. Alinibatiza katika imani, kanisa la Baptisti ya kimishenari.

98 Basi angalia, humu ndani, sasa, kama sisi . . . kama—kama tukifikia Nchi hiyo ya mpakani, tuseme, "Vema, utukufu kwa Mungu, nilinena kwa lugha, haleluya." Hilo silo. Kama unaweza kusema, ukose kuamini lolote la Neno hilo, kuna kasoro fulani na ujuzi wako. Unaona?

99 Unakuja moja kwa moja hadi kwenye Nchi hiyo na kuona ipo. Unaona kwamba Yesu amefufuka. Yuko miongoni mwetu. Unalisikia Neno linalofuata ujumbe, na ungali huamini Hilo, unajua kinachotokea? Basi walikufa moja kwa moja jangwani. "Kama tukitenda dhambi makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Hilo ndilo Kitabu cha Waebrania kinatuambia.

100 Na sasa angalia, wakati tukiziona ishara kuu za wakati wa mwisho duniani, ambazo Yeye aliahidi, jinsi gani zaidi inavyotuonya kwamba wakati umewadia. Achaneni na kutokuamini. Jiungeni pamoja. Tunapaswa kupendana mmoja na mwenzake na kuamini, na kujitenga na ulimwengu.

101 Angalieni, hawakupaswa tu kuja pamoja na kuzungumza juu ya ujumbe. Walipaswa kuingia ndani yake, kuingia chini ya damu. Sio kuja kusema, "Wajua, Musa alitwambia. Mjumbe, alisema, alitwambia kwamba inatupasa kuwa na damu. Mnawaza nini juu ya hilo, jamani?" Hilo halikuwa ndilo. Mwue mwana-kondoo huyo, halafu uiweke damu hiyo pale juu!

102 Tunaweza kuja na kuketi na kukubaliana na Neno, na kila kitu kingine, bali hatuna Ishara hiyo, inatufaidi nini? Hamna faida. Ingia chini Yake. Hakuwajibikia yeyote aliyekuwa nje kutoka chini ya damu hiyo. Wala Yeye hawajibiki kwa yeyote, leo hii, aliye nje kutoka chini ya Ishara.

103 Familia nzima, walikuwa tu salama walipokuwa chini ya ishara, nayo ishara iliwekwa hadharani. Familia yote! Je!

mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Leo hii tunapaswa kulikumbuka hilo, enyi watu. Watoto wetu!

104 Na huu utineja wa upuuzi na roki, na mambo tunayopitia, na hawa hapa Kundi la roki na wadudu, na je! mnajua kuwa yote imewakilishwa hapa kwenye Kitabu, cha Biblia? Inasema hivyo katika Ufunuo. Hakika, inasema. Jinsi ambavyo watu, wao, wao ni—wao ni . . . wao, wao, mnaona, wao, wao si . . . Wamekufa. Hawawezi kufufuka. Hawakuwa wa Milele kamwe. Hata hawakuwa kwenye Wazo, kwa hiyo wataangamia. Wataangamia milele, wameangamizwa kabisa. Wataadhibiwa kwa kipindi kirefu cha wakati kisichopimika, kwa kile walichofanya, bali chochote kilichokuwa na mwanzo kina mwisho.

105 Ni kile kisicho na mwanzo, hakina mwisho. Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Aina moja ya Uzima wa Milele, tunajitahidi tupate hiyo. Angalieni.

106 Yoshua, mlango wa pili wa Yoshua, kahaba Mmataifa aliyeamini alikuwa amesikia, pamoja na familia yake, na kuwaleta chini ya ukanda mwekundu, ambao ulikuwa ni ishara kutoka kwa wajumbe wa Yoshua. Malaika wa kuangamiza wa Mungu aliiheshimu ishara hiyo, na hiyo pekee, katika mji huo. Kulikuwa na kilichohitajika na Mungu, na watumishi Wake, kwamba Mungu alihitaji ishara hii, na hiyo ilikuwa ndiyo pekee. Sijali kama ilikuwa ni meya wa mji, kama ilikuwa ni mtu mtakatifu kuliko wote mjini, kama walihudhuria kanisa kubwa kuliko yote mjini, kila kitu kwenye mji huo kilianguka isipokuwa nyumba hiyo. Mungu, pekee, aliiheshimu ishara hiyo.

107 Angalieni, Yeriko ilikuwa imesikia kwamba Mungu alikuwa akifanya mambo makuu, bali hawakujali onyo hilo.

108 Ndivyo na watu leo hii wamekuwa wakisikia kile ambacho Mungu amekuwa akifanya kwa miaka michache iliyopita, bali hawatajali hicho. Uweza huu mkuu wa neema na ishara, kama Yeye alivyoahidi, “kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa.” Jinsi alivyoahidi jambo hilo lingekuwa! Angalia kilichotukia Sodoma. Kumbukeni, kulikuwa na ishara ya Sodoma. Bali mjumbe, wa Malaki 4, anapaswa “kuirudisha mioyo ya watu kwa baba zao, baba wa kipentekoste, kurudi kwenye Biblia.” Hakuwezi kuwa na zaidi ya Biblia, kitu kingine. Hii ndiyo ufunuo mkamilifu wa Mungu.

109 Naye mtu fulani anasema, “Vema, ninaamini sehemu *hii*, sijui kuhusu Hiyo.”

110 Mjumbe halisi wa Mungu na akurudishe moja kwa moja kwa Kitu hicho chote! Unaona? Angalia, hivyo ndivyo Roho Mtakatifu afanyavyo, kukurudisha kwa kila Neno la Mungu.

111 Neema Yake ilikuwa imeonyeshwa, Hukumu Yake ilikuwa inafuata. Hapana shaka waliamini kwamba walikuwa salama katika majengo yao makubwa ya kimadhehebu waliyokuwa nayo huko Yeriko, bali waligundua kuwa hayakufanya kazi.

112 Hapana shaka kulikuwa na baadhi ya. . . labda waliingia humo ndani kwa njia fulani, kulikuwa na wavulana kadhaa walioingia humo, wakaambiwa walete pamoja mbegu zote teule. Na mwanamke huyo aliweka. . . naye aliitumia nyumba yake kama kanisa, na kuwapokea wajumbe; ndipo basi akawaleta wote katika mji wake, walioweza kuamini, chini ya ishara.

113 Mwanamke mmoja katika taifa hilo kubwa lote! Maskini mwanamke mmoja, naye akiwa ni mwenye sifa mbaya, labda alitengwa na kila kanisa mjini, bali alimwamini mjumbe huyo. Naye mjumbe huyo akaacha ishara, alama, naye Mungu akaiheshimu ishara hiyo. Ndivyo ilivyo leo hii. Kumbukeni tu, wakati ghadhabu ya Mungu iharibuyo ilipokuja, mfumo huo mkubwa uliporomoka, ishara iliiweka salama nyumba ya mwanamke huyo. Si kwa sababu alikuwa ni mwanamke mwema; kwa sababu alikuwa na imani na aliiweka ishara.

114 Sasa vipi kama angalisema, "Naam, hao walikuwa ni watu wema, kwa kweli nilifurahia ujumbe waliotoa. Lakini, kwa kweli, kidogo inasikika ya kipumbavu kuwa na ukanda huo ukining'inia kutoka kwa dirisha langu. Nitauvuta tu ndani." Ingeanguka. Ingeanguka. Mungu aliiheshimu tu ishara, sawa na ishara ya uhai ilivyo huko Misri.

115 Yoshua alikuwa ni mfano wa Yesu, kwa sababu *Yoshua* maana yake "Yehova-mwokozi." Alikuwa ni mfano wa Yesu, alikuwa mwaminifu kwa alama ya ishara mjumbe wake aliyokuwa amehubiri. Yoshua alidumu mwaminifu kwa alama hiyo ya ishara. Wote chini yake waliokolewa, huko Misri. Wote chini yake waliokolewa, huko Yeriko.

116 Damu ya mwana-kondoo ni mfano leo hii ya Ishara, kwamba Roho Mtakatifu ndiye Ishara leo hii. Wote chini Yake wako salama. Wote ambao hawako chini Yake hawako salama. Katika Waebrania 13:10 na 20, Yeye anaitwa "agano la milele." Agano la kale lilikuwa kitu kimoja, hili ni Jipya, hili ni "agano la milele."

117 Mungu, ahadi za Mungu zinazofungamana na Damu, hutuweka huru na dhambi na aibu, na tofauti na ulimwengu mwingine wote. Haikulazimu kuvalia tofauti; mtu yeyote anaweza kuvalia tofauti. Inakubidi kuwa, ndani yako, tofauti. Uhai uko ndani; si mavazi, kuvalia. "Ufalme wa Mungu si chakula na kinywaji, au kuvaa nguo; bali ni uvumilivu, wema, upole, subira, katika Roho Mtakatifu."

118 Sasa, ahadi hizo hukuweka huru na dhambi, zinaonyesha kwamba Mungu haja—hajatambua dhambi yako. Daudi alisema, "Amebarikiwa mtu yule ambaye Mungu hatamhesabia dhambi." Naye Mungu hatahesabu dhambi juu ya hiyo Ishara, kwa sababu Ishara ni ushahidi wa malipo ya kwamba Mungu tayari ameipokea. Nawe una ishara kwa ajili yake, ghara-. . . imani yako imeinunua. Nawe una thamani ya kununua wokovu wako

ndani ya mwili wako, kumwabudu Yeye na kuzionyesha ahadi Zake na nguvu.

119 *Agano Jipya* humaanisha "mkataba mpya." *Damu* inamaanisha "Uhai." Agano Jipya ni agano la Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu akitoa ushuhuda ya kwamba Yesu Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, akionyesha kuwa Yesu ametimiza kila sharti kwa ajili yetu, na yu hai leo. Ishara inathibitisha Yeye yu hai kujitambulisha Mwenyewe pamoja nasi, kulingana na ahadi Yake. Sasa mtu anawezaje kusoma Biblia na kuona kwamba aliahidi hilo, na kumwona Kristo akirudi katika siku hizi za mwisho katika umbo la Roho Mtakatifu na kujitambulisha Mwenyewe kuwa hai? Hiyo ni Ishara. Hiyo ni alama. Hiyo ndiyo gharama iliyolipwa.

120 Kamwe, usitegemee mhemko fulani. "Nilihisi baridi ikipitia mgongoni mwangu. Na—nami ni—nilinusa kitu fulani; nikaona damu fulani mikononi mwangu, ama mafuta fulani. Ama—ama, nilipata Digrii yangu ya Kwanza ya Sanaa. Ama, nilicheza katika Roho. Nilipaza sauti. Nilinena kwa lugha." Mambo hayo huenda ni sawa. Sina kitu dhidi yake, bali hayo siyo ambayo ninazungumzia.

121 Ninazungumza kuhusu kutambulishwa kwa Ishara, Yesu Kristo, aliyefufuka na aliye ndani yetu sasa, akijitambulisha Mwenyewe, ili kuthibitisha tena Neno Lake lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii. Amina. Ndipo wewe na Kristo ni kitu kimoja. Mungu na Kristo ni mmoja. "Siku hiyo, mtajua ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Huyo hapo Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, akijionyesha Mwenyewe kuwa hai, baada ya miaka elfu mbili. Hiyo ndiyo Ishara.

122 Kama huko ndani, ingia ndani upesi sana, enyi marafiki. Huenda ikapata kuchelewa mno. Hatujui.

123 Kuonyesha Uwepo Wake, Agano Jipya, Damu. Na Hiyo ni hai sasa, ikifanya mathibitisho. Na kwa sababu Yeye yupo, tuna haki ya yote aliyotununulia Yeye. Mwanamume aliye na ubatizo wa Roho Mtakatifu, ama mwanamke aliye na ubatizo wa Roho Mtakatifu, ana haki kwa kila kitu ambacho Yesu alitununulia, kwa kuwa hiyo ndiyo ishara tuliyo nayo. Hiyo ndiyo uwezo wa kununua.

124 Labda kwa mfano unasema, "Vema, Ndugu Branham, unamaanisha nini?"

125 Hapa, kulifanya dhahiri sasa, nami nawatakeni nyinyi watu wagonjwa mpate hili. Angalia, kama nilikuwa ninakufa njaa, nami ninajua mkate boflo, tuseme, inagharimu robo, kisha moja kwa moja anakuja ndugu na kusema, "Hii hapa robo, Ndugu Branham. Una njaa; chukua hii robo." Sasa, unajua, ninaweza kuwa tu na furaha nikiwa na hiyo robo mkononi mwangu kama ninavyoweza kufurahia nikiwa na mkate mkononi mwangu,

kwa sababu nina thamani ya kununulia. Ninayo ishara ambayo hununua mkate. Na huo hapo mkate; na kitu cha pekee, ninashikilia ishara, robo ambayo hununua mkate, ninaweza tu kuwa na furaha nikiwa na hiyo ishara kama ninavyoweza kuwa nikiwa na mkate.

126 Sasa, kama una ubatizo wa Roho Mtakatifu, hiyo ndiyo Ishara kwamba unacho kila kitu cha ukombozi ambacho Yesu alifia, ni chako, kiko mkononi mwako. Je! unaogopa kukidai?

127 Nikiiweka mfukoni mwangu, na kusema, "Vema, sijui kama ninaweza kuununua ule mkate au la," nitakufa njaa. Lakini kumbukeni, mwuzaji anasema, "Nina hitaji moja tu, Bw. Branham. Senti ishirini na tano tu, unaweza kupata mkate boflo." Ninazo! Amina. Hilo latosha.

128 Hiyo ndiyo sababu hatuoni mambo mengi yakifanyika leo hii, Ishara haijawekwa hadharani, ile Ishara halisi. Loo, tuna kila namna ya bandia, bali ninamaanisha Ishara halisi.

129 Angalieni, ndipo wakati tunapotambua na kuwasilisha Ishara, Uhai uliohitajika kwa ajili ya Ishara, Damu hutunenea. Kumbukeni, Damu ya agano ilitambulishwa na Ishara, nalo Neno hutuhakikishia ahadi. Ishara ndiyo ushahidi kwamba gharama imelipwa kwa ajili yetu.

130 Sasa, ikiwa hujajumuishwa katika hilo, vema, bila shaka, hutapata chochote; unatembea tu kupitia mstari wa maombi, ukitembea kurudi na kutoka; unatembea hadi madhabahuni, na kuangalia juu, unatembea kurudi nyuma na kutoka.

131 Lakini, loo, ndugu, wakati Ishara hiyo ikipata kuwekwa ndani ya moyo wa—wa—wako, nawe unajua ni ufufuo wa Yesu Kristo ndani yako, jambo fulani linatukia. Hakuna kitu kitakachokugeuza. Unajua mahali pako. Utiifu mkamilifu kwa Neno lote la Mungu hukustahilisha Ishara, na hakuna chochote kingine. "Heri ni yule atimizaye Amri Zake zote, aweze kuwa na haki ya kuuendea huo Mti wa Uzima."

132 Halafu, tunapoomba, sharti tuwe na Ishara ya kuwasilisha pamoja na maombi yetu. Sasa usikose kupata hilo. Unapoomba, sharti uwe na Ishara kushikilia juu ya maombi yako; kama sivyo ulivyo, endelea kuomba mpaka Ishara ije, maana hujaahidiwa kuipokea. Unaona, huna budi kuwa na Ishara hii kwanza; hiyo ndiyo gharama ya kulipa, imani yako kuamini.

133 Sasa, ushuhuda wa utiifu mkamilifu. Hofu imeondoka. Paulo anatwambia kwamba, "Damu hunena mambo yaliyo mema."

Unasema, "Ati Damu hunena?" Naam, Damu hunena.

134 Katika Mwanzo 4:10, tunaona ya kwamba Mungu alisema kwamba—kwamba ninii ya Kaini... ama "Damu ya Habili ilinena kutoka ardhini." Tunaona katika Waebrania 12, kwamba, "Damu ya agano la Kristo hunena mambo mema kuliko ile ya Habili." Mnaona? Tunaona ya kwamba, Damu

hunena, hunena kwa niaba yako. Uhai uliomo ndani yako hunena kutoka kwa Damu iliyomwagika. Amina. Loo, ndugu! Laiti kila mtu angaliona hilo. Mnaona? Kama unaweza kuona kuwa ni nini, ni Uhai ulio ndani yako. Unaona, Damu hiyo inakutambulisha na Hiyo. Ni Ishara. Ninii . . . Kile kilicho, Damu ilimwagwa kwa ajili yako; umekubali, nao Uhai umekuja ndani yako. Unayo Ishara, hiyo ni Roho Mtakatifu.

135 Ndipo wakati tunapoomba, ni sharti tuwe na Ishara kuwasilisha pamoja na maombi yetu, kama nilivyosema, na sasa kuamini kwa ajili yetu na kuiweka Ishara kwa familia nzima, kama vile huko Misri, Yeriko, ama pia katika Matendo 16:31. Tunaona kwamba Paulo alimwambia akida wa Kirumi, kasema, "Wewe amini, na nyumba yako yote itaokoka." Iweke kwa familia yako. Kama unaye mtoto asiyeokoka, weka Ishara moja kwa moja juu yake, useme, "Bwana Mungu, ninamdai." Kaa papo hapo. Kama una mama ama mpendwa aliyepotea, weka Ishara hiyo juu yao, useme, "Bwana Mungu, ninaudai."

136 Toka nje, ya takataka zote za ulimwenguni, kutoka nyumbani mwako, jitayarishe kwa ajili ya Hiyo. Ziteketeze kaptura zako. Zitupilie mbali mbao zako za karata. Ziondoe sigara zako. Tumbukiza kutokuamini kwako na makaratasi yako ya kanisa kwenye pipa la takataka, palipo mahali pao. Amina. Basi unajiweka tayari. Halafu unafanya nini? Kisha uweke Ishara katika maombi, pamoja na thibitisho halisi, imani halisi. Iweke, iweke kwa ujasiri. Unapoiweka Ishara, fahamu kwamba umetakasika. "Ikiwa mioyo yetu haituhukumu, basi tunapata haja yetu."

137 Mradi nyinyi watu mnatenda mambo yasiyostahili, mtamwombaje Mungu kuwafanyia chochote huku mnajua mko makosani? Hiyo ndiyo sababu tunayumbayumba tu kwenda na kurudi tukiyumbayumba. Sisemi haya kuudhi. Ninasema haya ili kunyosha, kuweka mambo sawa. Utalijengaje juu ya vifusi vya Sodoma na Gomora? Rudini!

138 Mashirika na wahudumu wamewaacha watu kufanya chochote, na kuepuka, na kuweka tu jina lao kwenye kitabu na kuwaita *hili*, *lile*, na *linginelo*, wakati ni aibu. Na imefikia ambapo imani ni kitu ambacho hata si . . . hata hujui hata kidogo kwamba ni nini. Wao, wana tumaini, bali si imani.

139 Inakubidi kurudi, kwenye, kila kitu kimechambuliwa kabisa na ni safi. Ndipo uchukue Ishara yako, ambayo unajua ni Yesu Kristo ndani yako, halafu uiweke kazini. Jambo fulani lisipotendeka, kuna kasoro fulani; rudi nyuma tena, unacho kitu kisichofaa mkononi mwako. Yeye aliahidi hilo. Yeye Ndiye aliyeahidi hilo. Iweke kazini. Soma Waefeso 2:12, wakati fulani, ukipenda, nawe utaona hapo.

140 Angalia katika Waebrania 9:11, pia. Paulo alisema, "Nikimtumikia Mungu aliye hai, kwa mafundisho yaliyo hai."

Si kusema tu kama vile ningeenda kama Mwebrania alivyozoea kwenda, anachukua kafara yake, kisha anateremka barabarani, akiwa na fahali mkubwa mnene, na kuweka mikono yake juu yake na kujitambulisha, na kumwaga damu, anarudi amehesabiwa haki. Yehova alihitaji hiyo. Aliihitaji. Halafu kizazi kilichofuata, labda waliingia baridi zaidi; mtu mwingine, aliingia baridi zaidi. Muda si muda mwajua, likawa ni desturi ya familia.

141 Hivyo ndivyo pentekoste imekuwa kwetu, desturi ya familia. Tunashuka, tunasema, "Kipindi kile cha televisheni si kilikuwa cha kupendeza sana usiku wa leo? Siju walifanya nini huko chini kanisani? Bwana Yesu, ponya . . . " Loo, rehema! Mnaona? Ni destu- . . . ya familia. "Mnajua, nilinena katika lugha hivi majuzi. Mimi ni mshiriki wa *hili*, au *lile*, wajua. A-ha." Loo, ni desturi ya familia!

142 Unajua alichosema Mungu? Mungu alisema, "Mafuta yenu na kondoo dume wananuka katika pua yangu. Hiyo ni kweli, sadaka zenu zimekuwa uvundo."

143 Vivyo hivyo na sadaka za Pentekoste, na ugomvi wetu wote wa kimadhehebu na kufanya yasiyofaa, na wanawake wetu na wanaume kufanya jinsi wanavyofanya, mfano wa utauwa; kuuchochea muziki, na mtu fulani kuruka-ruka kwa kitambo; halafu yote imeisha, kama ilimwagiliwa ndoo ya maji, iwapo Neno la Mungu litatokea kuwa limekuja na kusema jambo fulani. Kuna shida gani? Sadaka zenu zimeanza kunuka mbele za Yehova.

144 Basi ilikuwa ni kwenye wakati huo ambapo Isaya alitokeza jukwaani, na kuwaambia, "Nitawapa ishara ya milele, bikira atachukua mimba." Mnaona, haya basi. Si desturi zilizokufa na kanuni za imani, la; bali mafundisho yaliyo hai, Mungu aliye hai aliyefufuka kutoka kwa wafu, na yu hai miongoni mwetu.

145 Baadhi yao, makanisa haya namna hiyo, yanayoamini mambo haya, yanakana kwamba kuna kitu kama Ishara. Vema, jamaa fulani alijaribu kuniambia, "Mitume kumi na wawili pekee ndio waliopokea Roho Mtakatifu. Walikuwa ni hao tu. Naam." Loo!

146 Bali sisi tunaoamini Neno, tunajua tofauti, tunajua kuwa huu ndio Uwepo ulio hai. Kwa kuwa tunajuaje kwamba ni Uwepo ulio hai wa Kristo, Roho aliye miongoni mwetu? Hufanya jambo lile lile Yeye afanyayo. Huo ndio ushahidi wake. Mzabibu hujulikana kwa matunda unaozaa. Ndipo basi kama ule mzabibu wa kwanza ulikuja nao wakaandika Kitabu cha Matendo nyuma yake, na jambo lile lile ambalo Yesu alitenda, wanafunzi walitenda; basi wakati mzabibu huo ukiinuka tena, unafanya jambo ile lile. Mnaona, Waebrania 13:8 inasema kwamba ni Yeye yule, loo, jamani, inathibitisha kwamba

Mungu amemfufua kwa ajili yetu, kulingana na Neno Lake lililoahidiwa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

147 Muhuri wa ahadi! Waefeso 4:30 inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Si hadi uamsho ujao. "Hata siku ya ukombozi wenu!" Mkibatizwa ndani Yake, kulingana na Wakorintho wa Kwanza 12. Na ndani Yake ni utimilifu, wala hakuna dhambi iliyoonekana ndani Yake. "Yeye aliyezaliwa na Mungu, hatendi dhambi. Mbegu ya Mungu inakaa ndani yake, naye hawezi kutenda dhambi." Anawezaje, huku Ishara ikiwa pale? Ishara ni ushahidi kuwa amekubalika.

148 Pia, vema, unasema, "Mimi hutenda dhambi." Vema, basi kamwe hujakuwa na Ishara. Unaona?

149 Ishara ndiyo kizuizi, inaonyesha kwamba gharama imelipwa. Shetani akijaribu kukukabidhi . . . Wazia tu hili. Shetani akijaribu kukukabidhi ugonjwa fulani, ama akijaribu kukukabidhi kitu fulani, je! unajua cha kufanya? Mwonyeshe Ishara yako. Hakika, ugonjwa humpiga Mkristo. Mwonyeshe Ishara yako, na kumthibitishia kwamba wewe ni bidhaa iliyonunuliwa ya Mungu. "Mpingeni shetani, naye atawakimbia." Shikilia Ishara juu ya imani yako isiyotikisika katika Neno Lake lililoahidiwa.

150 Mungu wakati mmoja alitoa alama ya upinde wa mvua kuwa ishara. Ninafunga. Alitoa alama ya upinde wa mvua kuwa ishara. Nina yapata tu dakika kumi, na halafu kuwa na mstari wa maombi. Alidumu mwaminifu kwa ishara hiyo. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Angali mwaminifu. Maelfu haya yote ya miaka, Yeye bado kamwe, hata wakati mmoja, hajashindwa kuiweka hadharani. Alikuwa mkweli kwa ishara hiyo, inatuonesha kwamba Yeye daima . . . wala kamwe hatakosa kuheshimu ishara Zake. Sijali kama ni . . .

151 Yesu asipokuja kwa miaka elfu kumi, mnayo Ishara, bado inampasa kuiheshimu. Haidhuru ni mambo mangapi yanayobadilika, na chochote kile, hana budi kuiheshimu hiyo Ishara. Yeye alisema ataiheshimu. Vema. Anatutarajia sasa kuionyesha Ishara Yake, juu ya imani yetu tuliyopewa na Mungu, kwa kila kundi potofu lisiloamini nchini na ulimwenguni, linaloamini kwamba ishara na maajabu hayafuati waaminio. Na kuwa mkweli kwa Ishara hii, Nayo inaonyesha kwamba nauli imelipwa nasi tumekubalika kwa ajili ya ufufuo, tukiwa na Uhai wa Ishara ndani yetu.

152 Huo ni ujumbe unaokata, bali ni Kweli. Hiyo ndiyo tunayohitaji, ni Kweli. Mungu tusaidie kuijua Kweli. "Mtaijua Kweli, nayo hiyo Kweli itawaweka huru." Ninadai kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninaamini kwamba Mungu hutoa Roho Mtakatifu kama Ishara, sasa hivi, kabla tu ya kutoka, kwa—kwa Bibi-arusi kutoka kwenye kanisa.

153 Ninaamini kuna upuuzi mwingi, na watu kusema walipaza sauti, walinena katika lugha. Ninaamini mambo hayo; lakini huwezi kutegemea hayo. Unawezaje kutegemea hayo, na halafu ulikane Neno? Mnaona?

154 Ishara ni Neno likitambulishwa ndani yako, ikiishi Yenyewe. Huyo ni Mungu akijifasiria Mwenyewe. Haikulazimu kusema, "Vema, sasa, wewe fasiri ndimi zangu." Hilo silo. Yeye hufasiri maisha yako kwa Neno. Yeye akilichukua neno lako, kile ulicho, na kulitambulisha Neno Lake kupitia hapo, hakuna haja ya fasiri yoyote, tayari ipo. Mungu hujifasiria Mwenyewe, nasi tutakuwa na ahadi hizi kwa ajili ya siku hii.

155 Loo, Dallas, enyi kundi la kupendeza la Wakristo, msichukuliwe na mambo haya ya siku hizi, mnayoona yakiendelea, maana yataangamia. Ionyeshe Ishara hiyo siku zote, iweke hadharani hiyo Ishara. Soma Biblia. Fikia kila kitu. Na kama roho yako ndani yako haisemi "amina" kwa Hiyo, basi afadhali urudi nyuma, ubadilishe hiyo uliyo nayo, kwa Ishara; hujapata Hiyo.

156 Ninajua hayo ni mengi sana kusema hapa alasiri moja. Na hivi sasa ni saa kumi u nusu. Ni wakati sasa, na kama tunaweza kutoka ifikapo saa kumi na moja pamoja na mstari wa maombi.

157 Je! mnaamini ya kwamba Yesu Kristo anaishi na kutawala leo hii? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini yale niliyowaambia kuwa ni Kweli? ["Amina."] Ndiyo Ishara, inayohitajika. Ninaweza tu kunena kilicho Kweli. Ninanena tu kile nionacho, ninachosikia, kilichofunuliwa kwangu. Na sababu yangu ya kusema hili; kati ya makumi ya maelfu mara maelfu ya nyakati, hakuna hata wakati mmoja imewahi kukosa kuwa kweli. Sasa hiyo haina budi kuwa ni Mungu. Hiyo haina budi kuwa ni Mungu. Vema, je! Mungu angeweza kumpa huduma kama hiyo mtu ambaye hajui kile anachozungumzia? ["La."] Hivi angejitambulisha Mwenyewe kama huyo mwonaji hapo, na kisha ageuke na kumpa Neno lililochanganyishwa? ["La."] Jamaa anayekataa Hilo, ndiye aliyechanganyikiwa. Wala Mungu hajachanganyikiwa. Mungu ndiye anayejifasiria Mwenyewe.

158 Pokea Ishara! Usiegemee kwenye kujiunga na kanisa lolote au mapokeo yoyote, au chochote. Pata Ishara! Shikilia Hiyo. Ndiyo kitu cha pekee ambacho Mungu atatambua. Ukifika kwenye wakati ule, ikifikia kifo chako, heri ushikilie hiyo Ishara juu yako; ukijua ya kwamba katika siku ya kuja Kwake, ule ufufuo, ninaweza kuiwasilisha hiyo Ishara. Haitakuwa katika mwili huu, huu umeoza; bali katika huyu Roho, asiyeweza kufa, ni Uzima wa Milele, Ishara hutulia hapo. Naye aliahidi, "Nitamfufua tena katika siku ya mwisho."

159 Yesu Kristo yuyo huyo yupo hapa. Yeye ndiye Mjumbe. Yeye ni...Huu *hapa* Ujumbe, na Yeye ndiye Mjumbe hapa

kuutambulisha Ujumbe Wake. Mimi siye Mjumbe. Yeye ndiye Mjumbe, na *Huu* ndio Ujumbe. Basi ikiwa una roho inayopingana na *Huo*, inawezaje kuwa ni Mjumbe wa Ujumbe? Ishara pekee ndiyo itakayoutambulisha. Amina.

160 Ninajisikia wa kidini. Kweli najisikia hivyo. Ninajisikia kama ninaweza kupaa niende sasa hivi, kwa kuwa ninamjua Yule niliyemwamini, na nimeyaona maisha yangu yakitambulishwa na Yeye katika Kufufuka Kwake. Uwepo Wake upo hapa. Ukubalini, enyi marafiki, tafadhali upokeeni, chini katika moyo wenu.

161 Ninajua sote tunakuja huku juu kuzunguka madhabahu na kuomba. Hilo ni wazo la kale la Kimethodisti. Kamwe hawakufanya hivyo katika Biblia. Biblia ilisema, "Wote walioamini walibatizwa." Hiyo ni kweli. Hakuna kitu kama mwito wa madhabahuni katika Biblia. Hicho ni kitu tulichoongeza, ambacho ni sawa. Chochote Mungu anachobariki, ni sawa.

162 Kama vile wanavyotia nguo mafuta. Hakukuwepo na kitu kama hicho katika Biblia. "Walichukua kutoka kwa mwili wa Paulo leso na nguo."

163 Lakini njia yoyote ile unayotaka kuifanya, ni sawa, kitini mwako, madhabahuni, popote pale. Jambo la pekee, iweke Hiyo, Ishara kwako. Halafu ujiangalie mwenyewe, na uone ni aina gani ya maisha yanayoendelea, uone kama Hiyo imewekwa kazini au bado. Ikiwa haijawekwa kazini, basi weka chochote ulicho nacho, kando, na urudi, mpaka Ishara itakapowekwa kazini.

164 Na tuombe. Baba wa Mbinguni, labda ni—ni—nimenena kwa pupa, lakini, Bwana, msumari utawezaje kushika isipokuwa uupigilie? Ninaomba, Baba, kwamba utapigiliwa ndani ya moyo wa watu, kusudi waweze kuona kwamba si jambo lolote la ubishi. Si kwamba ninajaribu kutambulisha shirika fulani, ukoo fulani, dhehebu fulani, mtu fulani, ama mimi mwenyewe, au mtu yeyote mwingine. Ni Yesu Kristo. "Nitayaweka madhehebu hayo yote pamoja," hayo ni sita kwa dazani moja na nusu ya lile lingine, kulingana na Neno Lako. "Maskini mama kahaba," Biblia katika Ufunuo 17, "alikuwa ndiye mama wa kila mmoja wa hao makahaba." Basi wasingeweza kuwa ni wanaume. Walikuwa makahaba, nao wote waliingia katika kitanda cha ulimwengu. Nasi tunaona imefanyika hivyo, Wapentekoste na wote.

165 Bali, Yesu, ungali unabaki Yesu. Jalia wasisikilize ujumbe wa kanisa; ila Ujumbe wa Kristo, Neno. Naomba ujitambulishe Mwenyewe, Bwana, leo hii, pamoja na waaminio. Waponye wagonjwa wote. Samehe dhambi zetu, Bwana. Na—naomba, kama mtumishi Wako, naomba usamehe dhambi zangu, na usamehe dhambi za watu hawa. Ninatumaini, Bwana. Kila mmoja wao hapana shaka amesaidia katika matoleo, kulipia

ma—majengo, nao wametumia fedha zao, nao wame—wame—wamefanya kila kitu, Bwana. Ee Mungu, ninaomba ya kwamba hakutakuwako hata mmoja wao atakayeikosa, Bwana. Jalia kila mmoja.

166 Ni—ninafanya hayo kwa uaminifu, na hata hivyo, Bwana, lazima uwe mkali. Tunajua, kusahihisha ni upendo. Upendo husahihisha. Nami ninaomba. Kwa kuwa hiyo ndiyo sababu Wewe uliwasahihisha watu Wako, ni kwa sababu uliwapenda, na kila dhambi haina budi kujibiwa.

167 Pia, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utazisamehe dhambi zetu sasa, tunapoziungama. Tumetembelea mbali, Bwana. Ninatambulishwa na watu hawa Wapentekoste, Bwana. Mimi ni—ni mmoja wao. Nami na—naomba, Mungu, kwamba Wewe utatusamehe sote. Na uchukue baadhi ya hawa viongozi na kuwageuza, na—na kuwafanya waelekeze macho yao Kalvari huko wakati mmoja, na ndipo watasahau kuhusu kile kiwapasacho kuwa, mzee wa jimbo au askofu, ama chochote kile, na kujua kwamba sisi si mabwana wakubwa katika Ufalme huu. Sisi sote ni watoto wa Mungu. Ninaomba ya kwamba utatusaidia sasa. Jitambulishe Mwenyewe miongoni mwetu, leo hii. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

168 Sasa kabla tu hatujaanzisha mstari wa maombi, huenda kuna mtu hapa ambaye hajawahi kuwa hapa hapo kabla. Sijui wewe ni nani, bali Mungu anakujua. Kama nimesema Kweli, Mungu na aitambulishe, kama ni Kweli au la, hilo ndilo thibitisho lake. Kama amefufuka kutoka kwa wafu, ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Alisema katika Yohana 14:12, "Yeye aaminiye," si yule anayejifanya kuamini. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya pia." Hiyo ni kweli?

169 Mtu fulani alisema, "'Kubwa zaidi mtafanya.'" Hiyo ni kweli. Kasema, "Vema, tunahubiri Injili, hiyo ni kuu zaidi."

170 Yafanye tu mambo aliyofanya, hiyo itanithibitishia, unaona, ndipo tutazungumzia zilizo kuu zaidi. Ninaweza kukuonyesha mambo makuu zaidi anayofanya sasa kuliko aliyofanya wakati Yeye alipokuwa duniani, na hiyo si tu kuhubiri Injili, pia; hiyo ni katika ishara na miujiza. Hatuna wakati kwa hayo. Aminini tu. Na hebu Mungu wa Mbinguni, Yule aliyemfufua Yesu Kristo kutoka kwa wafu, na amemwasilisha hapa akiwa hai, kwetu, baada ya miaka elfu mbili, autambulishe Ujumbe huu, kwamba ni sahihi. Ishara haina budi kuwekwa kazini.

171 Sasa, nyinyi mlio na magonjwa na matatizo, ombeni, semeni tu kwa uaminifu, "Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe ni 'Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.' Nasi tunaambiwa na mhudumu huyu hapa, ya kwamba Wewe uko pamoja nasi, hapa, basi nakutaka Wewe uwe hapa

pamoja nasi na ujitambulishe Mwenyewe." Sasa ombeni, kila mmoja wenu.

172 Sasa ni jukumu la Mungu kusema jambo. Ni wakati wa jinsi gani! Loo, jamani! Laiti mngaliweza tu kujua jambo fulani, jinsi mnavyojisikia wakati Hiyo ikija, ulimwengu wote ni wako. Amina. Hakuna pepo atakayetenda chochote, yeye ni kiumbe kilichoshindwa. Bwana wangu yupo. Yote yako mikononi mwetu. Amina.

Tafadhali iweni kimya kabisa. Msitembee. Kaeni kimya.

173 Nyinyi kwenye viti vya magurudumu, na kadhalika, msidhanie kuwa hamjiwezi. Aminini. Wewe—wewe, umepitia kwenye mistari ya maombi, na umeshindwa na kushindwa. Haikuwa ni mhudumu aliyekuombea, aliyeshindwa. Ni imani yako, nawe umeanza kuwazia kuwa hutafanya lolote. Wewe amini.

174 Hapa, hii hapa Nuru hii hapa, juu ya maskini mama mweusi anayeketi hapa nyuma, aliyesimama huku ameinua mikono yake *hivi*. Naam. Ulikuwa unaomba. Naam. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, au mtumishi Wake? Sipaswi kusema hayo, maana huwakwaza watu sana. Una ninii nzuri . . .

175 Huyu hapa mwanamume mzungu, mwanamke mweusi, kama tu ilivyokuwa Bwana wetu na yule mwanamke kisimani, jamii mbili tofauti. Aliwafanya wajue kwamba hakuna tofauti katika jamii. Rangi zetu hazina uhusiano wowote nalo. Sisi sote . . . Tunaweza kupeana damu mmoja kwa mwenzake. Mungu alifanya, wa damu moja, mataifa yote.

176 Una maumivu ya kichwa, maumivu makali ya kichwa. Halafu una mzigo moyoni mwako, huo ni kwa ajili ya yule mtoto. Na wewe . . . Anateseka. [Dada huyo anasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni kweli kabisa. Je! hiyo ni kweli? ["Amina."] Hiyo ni kweli.

177 Mama huyu anayeketi karibu na wewe hapo, anaonekana kutambulishwa na wewe, ambaye ni mama yako. [Dada huyo anasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni kweli. ["Mungu asifiwe!"] Naye ana shida fulani.

178 Je! unaniamini, mama? [Mama anasema, "Amina."—Mh.] Unaamini? Shida yako ni maumivu ubavuni mwako. Hiyo ni kweli. Ni ubavu wako wa kuume unaouma. Je! hiyo ni kweli? Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli. Haitakusumbua tena. Unaamini (ikiwa) Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? Bibi Lowell. ["Amina."] Sahihi. ["Amina."] Vema, nenda zako, Bwana Yesu anakupa haja yako.

179 Moja kwa moja kwenye mwisho pale yupo maskini mama mwingine mweusi ameketi, akiangalia, hiyo karibu—karibu imrarue vipandevipande. Ananiangalia moja kwa moja. Anaamini. Hicho, hamwoni Kitu hicho papo hapo karibu naye?

Anasumbuliwa na tatizo la figo. Hiyo ni kweli. Imekwisha sasa; Yeye amekuponya. Amina.

180 Mbona usiamini? "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hapa kuna . . . Waangalie watu weusi! Imani yenu iko wapi, enyi wazungu?

181 Huyu hapa mama mweusi ameketi moja kwa moja hapa, akiniangalia moja kwa moja, kwa namna fulani ni mama mnene. Ana shida kwenye goti lake. Pia ana tatizo, ana tatizo la moyo. Naam. Naye ana udhaifu, moyo kudunda upesi na mambo kama hayo, hasa unapojaribu kulala chini, kusongwa roho. Unaona? Hayo yalifanyika jana usiku. Kumbuka, siyasomi mawazo yako, bali ninajua kile ulichoombea. Ulitaka uitiwe jambo hili, leo hii, na Yeye amekujibu. Sasa pia ni vigumu kwako kusimama, kwa sababu una baridi yabisi. Hiyo ni kweli. Na halafu, kitu kingine, una ugonjwa wa tumbo, ambao ni uvimbe ndani ya tumbo. Hiyo ni kweli. Sasa je! unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Nitalisema, kwa vyovyote vile. Amini, nawe utaponywa.

182 Vipi kuhusu shida *yako* ya tumbo? Je! unaamini kwamba Mungu ataponya ugonjwa wako wa tumbo, unayeketi hapo, pia? Je! unaamini hilo? Vema, basi unaweza kuwa na uponyaji wako wa tumbo lako. Amina.

183 Unataka kuacha uvutaji wa sigara, hapo, mama? Unaamini kwamba Mungu atakufanya uache uvutaji sigara? Umekuwa ukijaribu kwa muda mrefu. Una shida ya tumbo, pia; umekuwa ukijaribu kuacha sigara. Hiyo ndiyo inayosababisha tatizo la tumbo lako. Je! utaziacha? Ninazipinga kutoka kwako, katika Jina la Yesu Kristo, kwa sababu ya imani yako kumgusa.

Ninakupa changamoto kumwamini Mungu!

184 Huyu hapa maskini mwanamke anayeketi hapo akiombea nanii wake . . . mpendwa wake kwenye hospitali, anayekufa, kwa kansa. Vema. Ni mjomba. Hiyo ni kweli. Ama wewe . . . Wewe ni mke wa mhudumu. Wewe amini kwa moyo wako wote, mtu huyo atapona.

185 Ninakupa changamoto kumwamini Mungu! Hiyo ni nini? Utambulisho, huyo Yesu Kristo. Unasema, "Kristo ni nini?"

186 Yeye ni Neno. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, Neno alikuwa pamoja na Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." "Neno ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Hivi huwezi kuona Neno limekuja miongoni mwetu katika siku za mwisho? Ni Roho Mtakatifu akichukua Neno la Mungu na kumtambulisha Yesu Kristo, ambaye ni Ishara. Amina. Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

187 Ni wangapi walio na kadi za maombi? Hebu wote upande *huu* walio na kadi za maombi, wasimame kwenye mstari huu

*hapa*. Simameni tu, wote upande ule, upande huo tu simameni hapa kwenye marefu. La, kwenye marefu ya upande wa kuume pekee, tafadhali, papo hapo. Mabawabu, nendeni mahali penu. Halafu wakimaliza, wengine wasimame, baada ya wao kupita, halafu vinginevyo na upande ule mwingine. Sasa hebu kila mtu awe na kicho.

188 Roho Mtakatifu alichukua mkutano, kwa hiyo kulikuwepo ya kutosha ambayo yamesemwa na kufanywa ili kuthibitisha. Ni wangapi wanaamini Yeye yupo hapa? Ni wangapi wanaamini hiyo ndiyo Ishara? Ni wangapi wanaamini ni Neno? [Kusanyiko linaanza kushangilia—Mh.] Angalieni, ni wangapi wanajua kwamba Kitabu cha Waebrania kilisema, kwamba, "Neno la Mungu huyatambua mawazo yaliyo moyoni"? Ni wangapi wanajua hilo? Ni wangapi wanajua kwamba hiyo ndiyo sababu Yesu angeweza kutambua mawazo yaliyo katika moyo wao, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno? Ni wangapi wanaamini hilo? Ni wangapi wanaamini kwamba hilo ndilo lililokuwa na manabii? Ndio waliojiliwa na Neno. Sasa Neno likiturudia sisi, si litafanya jambo lile lile? Basi Neno linalotambulisha Neno, linawezaje kukosea kwa Neno? Loo, rehema! Kicho!

189 We, mama huyu anayeketi hapa, analo jambo fulani moyoni mwake, pia. Ilitokea tu kwamba niligeuka na kulishika. Wewe si ni Bibi Grant? Sikujua hilo. Lakini wewe ni Bibi Grant, maana ninakuona nalo. Una hali ya wasiwasi inayokusumbua. Una, mwanao ana kitu fulani kingine. . . damu yake, ni kama, inadondoka. Ninakupa changamoto kuamini! Amina. Yeye ndiye Bwana wa hali hiyo. Ndiye Bwana wa mauti.

Na tuombe.

190 Bwana Yesu, huku Uwepo Wako ukitutia upako, hapa katika jengo hili, nasi tunajua huyu ni Roho Mtakatifu, ninaomba, Bwana, ya kwamba utamponya kila mtu atakayezivaa leso hizi.

191 Wakati mmoja, tunafundishwa katika Biblia, kwamba watu Wako, moja kwa moja kwenye wajibu wao, walikuwa wakivuka Bahari ya Shamu, nayo bahari ikawazuia, wakiwa njiani kuelekea nchi ya ahadi. Mungu aliangalia chini kupitia hiyo Nguzo ya Moto, kwa macho yenye hasira, nayo bahari ikaogopa, ikarudi nyuma, na Israeli wakaenda kwenye nchi ya ahadi, moja kwa moja kwenye wajibu wao.

192 Ee Bwana Mungu, naomba macho Yako yaangalie kupitia Damu ya Yesu Kristo, moja kwa moja kuingia kwenye Ishara hii hapa ambayo tunashikilia juu ya leso hizi leo. Pia naomba kwamba yeyote atakayevaa hizi, jalia ugonjwa utishwe, ukasonge nyuma na kuwaacha watu Wako wavuke kuingia kwenye ahadi ya afya njema. "Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa." Katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo. Amina.

193 Ni wahuhibiri wangapi waaminio wa Methodisti waliopo hapa, wahubiri wa Kibaptisti, wahubiri wa Kipresbiteri,

wahubiri wa Kibaptisti, wa Kilutheri, au Wapentekoste? Ni wangapi wenu wanaamini Hili kuwa ni Kweli? Njoni hapa na kusimama karibu nami wakati tukiwaombea wagonjwa basi. Njoni huku juu, nyinyi wahubiri wote mnaoamini.

194 Ni sawa, sivyo? Ndugu Grant, hiyo ni sawa? [Ndugu Grant anasema, "Hakika."—Mh.] A-ha.

195 Njoo hapa chini, ndugu. Ndugu Grant anayo huduma ya kuwaombea wagonjwa. Mtu hodari, mtu mwema, mtu ambaye Mungu humsikia na kujibu maombi yake, Ndugu Grant. Nina furaha kumkumbatia leo hii na kusema hayo, na ndugu yangu. Sasa atakuwa hapa chini akiomba pamoja nami.

196 Unapopitia mstari huu, kama tu ulikuwa ukija chini ya msalaba. Ndugu, pangeni mistari miwili papa hapa, papa hapa. Pangeni mistari miwili; baadhi hapa juu, wengine hapo chini.

197 Ndugu Roy Borders, uko wapi? Ndugu Roy Borders, nilifikiri alikuwa hapa. [Mtu fulani anasema, "Atarudi moja kwa moja."—Mh.]

198 Angalieni hapa, kwenye wahudumu, mtafanya hivyo! Angalieni pale. Hiyo hunifanya kujisikia vizuri, ndugu. Wahudumu wa msalaba, watu wanaosimama hapa kujitambulisha wenyewe na Ujumbe. Ni nini kinachoweza kutendeka?

199 Sasa, angalia, usiuweke juu ya wahudumu sasa. Wamekuja kujitambulisha. Unapopitia hapa, jitambu-. . .shikilia Ishara mbele zako, "Bwana Yesu, nimekiri dhambi zangu. Kama malipo, Wewe umenipa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mimi ni bidhaa iliyonunuliwa. Dhambi, ugonjwa au chochote hakiwezi kunishikilia tangu sasa na kuendelea. Ninasonga vizuri." Shikilia hiyo, loo, mbele zako, na upitie hapa, naye Mungu atakuponya nawe utatoka hapa ukishangilia, mwenye furaha, na utakuwa mzima. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

200 Sasa kila mtu humu ndani, hebu tuinamishe vichwa vyetu, ndugu, tukiwa pamoja. Hatujui kinachoenda kutendeka. Hatujui kabisa. Hakuna haja yoyote kwa mtu yeyote aliye mgonjwa kuondoka kwenye jengo hili alasiri ya leo. Shikilia Ishara hiyo moyoni mwako, pita moja kwa moja kwenye mstari huu wa maombi; ambapo wahudumu, ambao wameweka maisha yao wakfu kwa—kwa ajili ya huduma, watasimama hapa, wakiwawekeeni mikono mnapopita.

Unasema, "Ulifanya hivyo kwa sababu gani, Ndugu Branham?"

201 Ninawatakeni, kila mmoja, kujua kwamba ninii tu. . .Mimi siye mponyaji. Watu hawa wana haki ya kuwaombea wagonjwa kama mtu mwingine yeyote. Kusema kweli, ninaamini Mungu angejibu maombi yao kabla hajajibu yangu. Nimechoka na ni

mchovu, na kila kitu. Na—naamini ya kwamba Yeye angeyajibu maombi yao. Nao hawa hapa wamesimama moja kwa moja kati yake, kujitambulisha wenyewe, bila kuaibika kuchukua mahali pao. Ninawathamini watu kama hao.

202 Sasa, ndugu, ninajua hisia yenu. Mimi, mimi ni mmoja wenu. Mimi ndiye niliyeunganisha wavu wangu nanyi, hapa Texas, kujaribu kushika kila mmoja wa hao samaki ambao Mungu amewakusudia Uzima, huko nje. Ninafanya yote niwezayo. Niko pamoja nanyi, asilimia mia moja. Wakati mwingine ninakemea na kupaza sauti dhidi ya madhehebu na kadhalika. Hiyo haimaanishi kwamba ninawapinga, ndugu yangu. Ninamaanisha kuwa ninapinga mfumo ambao ungetutenga kutoka kuwa ndugu, kwa sababu ya mafundisho fulani ya kidini. Sisi ni ndugu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tunashikilia Ishara ile ile. Tumepokea Damu ile ile, kwa hiyo hebu tuamini hilo. Tunaweza kukutana Huko (sivyo?), ndugu, kila mmoja wetu chini ya Damu.

203 Sasa, niliwekwa wakfu Mbaptisti. Labda wewe ni Mmethodisti, ama Mlutheri, au Mpresbiteri, Mpentekoste, Umoja, Uwili, Utatu, ama chochote ulicho nacho, Church of God, chochote kile. Hiyo haileti tofauti yoyote. Hatuwezi kukubaliana juu ya mambo hayo madogo, hebu tusahau hayo basi.

204 Kitu fulani tunachoweza kukubaliana juu yake, kwamba Yesu Kristo Mwokozi wetu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, akafufuka tena na kutupa Ishara. Tunasimama hapa pamoja na maombi yetu, kushikilia juu ya ndugu hawa na dada wagonjwa wanaopitia kwenye mstari huu. Nitaamini kwa moyo wangu wote.

205 Niliona jambo fulani likitendeka papo hapo. Amina. Ninajua mnafikiri nina kichaa, bali ninajisikia vizuri na kichaa. Natumaini tu ninaweza kubaki namna hii. Naam, bwana. Ninajisikia vizuri sana hivi.

Na tuombe.

206 Bwana Yesu, ninaondoka kwenye mimbara hii, kutembea hapa chini, ili kujitambulisha na ndugu hawa. Ninajitambulisha nao, huku sisi sote tunashikilia Ishara zetu mikononi mwetu, na mioyoni mwetu. Huku tukitii amri Yako, "kuweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Jalia kila mtu anayepitia hapa, wawasilishe Ishara yao, kwamba wamepokea Roho Mtakatifu, kwamba wao ni mwana wa Mungu aliyezaliwa upya, kwamba wanaamini kwa moyo wao wote. Na wanapopitia, jalia waulaani ugonjwa huo na mateso ya mwili wao. Na jalia watoke hapa wakishangilia, wakijua kwamba imani yao imewaponya.

207 Pia, Bwana Mungu, kama tulivyoweka, Agano la Kale, mikono yetu juu ya kafara, kujitambulisha wenyewe na kafara, tunaweka mikono yetu juu ya Yesu na kujitambulisha na Yeye. Yeye aliweka mikono Yake juu yetu sasa katika

huduma, akijitambulisha Mwenyewe pamoja nasi, kwa ishara na maajabu. Nasi tunaweka mikono yetu juu ya wagonjwa, kujitambulisha pamoja nao, pamoja na imani yetu ikiunganishwa nao. Ugonjwa lazima uondoke, na jalia uondoke katika Jina la Yesu Kristo, tunapotembea hapa chini kuupokea.

Hebu kusanyiko lote liombe.

208 Roy au mtu mwingine aje hapa na asimame karibu na maikrofoni hii, na udumishe mistari ikiwa imenyoka.

209 Angalieni, mnapopitia hapa sasa, njoo ukiamini, njoo ukiomba. Tunaenda tu kuweka mikono juu ya wagonjwa. Pitieni moja kwa moja. Ombeni. Unapopitia mstari wa hawa wahudumu; kama unatembea kwa mikongojo, iweke chini na uende ukitembea. Kama umekuwa na kansa, ugonjwa, sema, "Daktari amefanya yote awezayo kufanya, amefanya yote aliyoweza, naye alisema itanibidi kufa. Sitakufa. Hii hapa Ishara yangu, Bwana. Umeniahidi sabini. Ninapitia moja kwa moja hapa, nikifanya hivyo." Mnaona, fanyeni hivyo. Je! mtafanya hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Katika Jina la Yesu, na iwe hivyo. Amina.

210 Vema, acha mstari upite. [Ndugu Branham na wahudumu wanawaombea wagonjwa, huku ndugu mmoja akiongoza kusanyiko katika kuimba *Amini Tu* na nyimbo zingine. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Naamini!
Mashaka yangu yote yamezikwa kwenye Chemchemi.

211 Je! mnaamini hayo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina. Loo, Yeye si ni wa ajabu? ["Amina."] Baadhi yao walikuwa kwenye vitanda hivyo vya wagonjwa na machela, walisimama moja kwa moja na kuondoka wakitembea; wakiviacha tu vimewekwa hapo, nao wakaondoka wakitembea. Loo, ni kwamba kila mtu anaweza kuponywa sasa, ambaye ataliamini. Je! mnaamini? ["Amina."]

212 Hebu tupe sauti, *Nampenda*, waweza, dada; ule wimbo wa kale, "Nampenda, nampenda kwani . . . "? Hebu sote tuinue tu sauti zetu, na mikono yetu, mioyo yetu, kwa Mungu, na tuimbe, "Nampenda, nampenda, kwani alinipenda kwanza." Kila mtu sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalva- . . .

213 Mama, amesimama kutoka kwa kiti cha magurudumu, anatembea kupitia hapa akisaidiwa na wanaume wawili. "Na . . . " Hebu tumpungie Mungu mikono yetu, "Nampenda!"

Nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari . . .

Hebu na tumsifu tu sasa, kila mtu!

214 Utukufu kwa Mungu! Jinsi tunavyokushukuru, Bwana Yesu, kwa ajili ya wema Wako, Uwepo Wako. Loo, tunakushukuru kwa ajili ya Ishara, Bwana. Tumeokolewa na kujazwa na Roho, Roho Mtakatifu akitapakaa miilini mwetu sasa. Jinsi tunavyokushukuru kwa hili, Baba! Loo, katika Jina la Yesu tunakushukuru. Amina. Amina.

215 Kila mtu peana mikono, useme, "Bwana asifiwe!" Peaneni mikono nyinyi kwa nyinyi, mseme, "Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!" (. . .?. . .) Vema, sasa, sote pamoja tena.

Nampenda, (mikono ikiinuliwa, mioyo imeinuliwa) na . . . (onyesha tu kutoka moyoni mwako)
Kwani alinipenda kwanza (Je! mtafumukana?)
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

216 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa uchaji sana, wakati nikigeuza ibada sasa kwa Ndugu Grant kwa ajili ya kufumukana; nikimshukuru kila mmoja wenu. Kwanza, nikimshukuru Bwana kwa wema Wake, rehema Zake, na hakikisho ambalo natumaini tumeacha mioyoni mwenu, kwamba hatupo hapa peke yetu. Jemedari wetu Mkuu yu miongoni mwetu. Kelele za Mfame zimo kambini. Nasi tunamshukuru Bwana, kuona nguvu Zake kuu na rehema Zake kuu. Na sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa uchaji. Ndugu Grant.

*Ile Ishara* SWA64-0308
(The Token)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 8 Machi, 1964, katika Soul's Harbor Temple kule Dallas, Texas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org